# Itikadi ya Maimamu wanne Mwenyezi Mungu awarehemu

## (Abuu Hanifa na Maliki na Shafy na Ibn Hambali)


**Aliye kiandaa**
**Kundi la Wanafunzi**

**Kimetangulizwa**
**Swalah Bin Muhammad Al-Budayri**

Imamu na Khatibu wa Msikiti Mtukufu wa Mtume Madina
na ni Hakimu wa Mahakama ya Mdina Al-Munawarah




# Itikadi ya Maimamu wanne Mwenyezi Mungu awarehemu

## (Abuu Hanifa na Maliki na Shafy na Ibn Hambali)

Aliye kiandaa: Kundi la Wanafunzi

Kimetangulizwa: Swalah Bin Muhammad Al-Budayri

Translation and Reviewing:
rwwad translation center

ⓒ دار العقيدة للنشر والتوزيع ، ١٤٤٣هـ

***فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر***

نخبة من العلماء
عقيدة الأئمة الأربعة رحمهم الله تعالى - باللغة السواحلية. /
نخبة من العلماء - ط١. .- الرياض ، ١٤٤٣هـ
١٢٧ ص ؛ ..سم

ردمك: ٩-٠٤-٨٣٧٠-٦٠٣-٩٧٨

١- التوحيد ٢- العقيدة الاسلامية أ.العنوان
ديوي ٢٤٠ ١٤٤٣/٧٣٣١

**رقم الإيداع: ١٤٤٣/٧٣٣١**
**ردمك: ٩-٠٤-٨٣٧٠-٦٠٣-٩٧٨**

(ملاحظة): لا يتم طباعة الجزء الأسفل مع بطاقة الفهرسة

تأمل مكتبة الملك فهد الوطنية تطبيق ما ورد في نظام الإيداع بشكل معياري موحد ، و من هنا يتطلب تصوير الجزء الاعلى بالأبعاد المقننة نفسها خلف صفحة العنوان الداخلية للكتاب ، كما يجب طباعة الرقم الدولي المعياري ردمك مرة أخرى على الجزء السفلي الأيسر من الغلاف الخلفي الخارجي .
**و ضرورة إيداع نسختين من العمل فى مكتبة الملك فهد الوطنية فور الانتهاء من طباعته، بالإضافة إلى إيداع نسخة الكترونية من العمل مخزنة على قرص مدمج (CD) وشكرا ،،،**

# Utangulizi wa Shekh Swalah Al-Budayri

Kila sifa kamilifu ni za Allah ambae aliehukumu akafanya uadilifu, kisha akahalalisha na kuharamisha, kisha akawafundisha waja wake wakajua sheria zake na akawafundisha elimu ya fiqihi katika dini wakajua nina shahidilia kuwa hapana mola apasae kuabudiwakwa haki ila ni mola mmoja hana mshirika, aliweka vizuri misingi ya dini kwa kushusha Kitabu chake kilicho pangiliwa vyema, ambacho ndio uongofu kwa ummah wote na nina Shahidilia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na ni mtume wake, ambae ametumwa kwa walimwengu wote, kwa warabu na waejemi kwa dini takatifu na sheria, kwa watu wanao paswa kuifuata na Mtume hakuacha kuilingania dini hiyo na kuibainisha kwa hoja na kuihami kwa hoja za mkato zinazo bainisha, rehma na amani za Allah ziwe juu yake na Masahabazake, ambao wanapita katika njia ya Mtume na baki ya wanao ifuata, Baada ya kusema haya:

Hakika nimepitia risala hii iliyo itwa (Itikadi ya Maimamu wanne Allah awarehemu) ambayo imeandaliwa na kundi la wanafunzi na nikaikuta ni yenye kuafikiana na Itikadi sahihi, ambayo imepita katika itikadi sahihi ya watu wema walio tangulia, ambayo imejengeka katika misingi ya Qur'an na

sunnahh.Na kwa umuhimu wa maudhui yake na yale yalio kuja ndani yake katika maswala mbali mbali, mimi nina husia kichapishwe na kusambazwa, nikiwa ni mwenye kumuomba Mwenyezi Mungu mwenye uwezo kimnufaishe kila mwenye kukisoma na Allah amlipe heri alie kiandaa naakakikamilisha na swala na amani ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad na ali zake na maswahaba zake wote.

Imamu na Khatwibu wa Msikiti wa Mtume
Ni hakimu wa Mahakama ya Mdina Al-Munawarah
Swalah Bin Muhammad Al-Budayri

# Utangulizi wa watunzi

Kila sifa kamilifu ni za Allah mola wa viumbe vyote, sala na salam ziwe juu ya Mtume Muhammad, bwana wa Mitume wote na juu ya ali zake na maswahaba zake wote, baada ya hayo tunasema:

Hii ni Risala kwa ufupi ikibainisha mambo amabyo yanayo pasa kwa Mwanadamu kujifunza na kuyaamini, katika mambo ya Tawhidi na misingi ya dini na baadhi ya mambo ambayo yanayo ambatana nayo, ambayo yamechukuliwa kutoka katika vitabu vya itikadi za maimamu wanne:

Imamu Abuu Hanifa na Imamu Maliki na Shafy na Imamu Ahmad Bin Hambal na wafuasi wao Mwenyezi Mungu awarehemu na wale walio jikusanya katika itikadi ya Ahlusunnahh waljamaa na hawakuhitalafiana,Kama vile kitabu cha Alfiqhu Al Akbar cha Abuu Hanifa Allah amrehem aliekufa (150H) Na kitabu Aqidatu Twahawiyah cha Imamu Twahawiyah aliekufa mwaka (321H) na amekisherehesha mwanachuoni Abil-Iziy Alhanafy aliekufa Mwaka (792H) Na kitabu: Muqadimatu Risalatu cha Ibn Abiy Zaidi Alqayrawany Almaliky aliekufa Mwaka (386H) Na kitabu: Usulu Sunnahh cha Ibn Abiy Zamanayni Almaliky aliekufa Mwaka 399HNa kitabu: Tamhiid sherhu almuwatwa'a cha Ibn Abdil Bari Almaaliky aliekufa Mwaka (463H).

Na kitabu: Risalah katika itikadi ya Ahlul Hadithi cha Swaabuny Ashafy aliekufa Mwaka (449H) Na kitabu: Sharhu Sunnahh cha Muzany mwanafunzi wa imamu Shafy aliekufa Mwaka (264H) Na kitabu: Usulu sunnahh cha Imamu Ahmad Bin Hambal, aliekufa Mwaka (241H) Na kitabu: Kitabu Sunnahh cha AbdAllah Bin Ahmad Bin Hambal aliekufa Mwaka (290H) Na Kitabu Sunnahh cha Khalal Alhambaly aliekufa Mwaka (311H) Na kitabu: Bida'a na makatazo yake cha Ibn Wadhwaha Al Andalosy aliekufa Mwaka (287H) Na kitabu Hawadithi walbida'a cha Abubakar Altwartuushy aliekufa Mwaka (520H) Na kitabu: Albaaithu Ala Inkari Albida'a walhawadith cha Shamah Almaqdisy Alshafiy aliekufa Mwaka (665H) Na vitabu vingine katika vitabu vya misingi na itikadi ambavyo vilitungwa na maimamu na wafuasi wao waliofuata ulinganio wa kweli na kuhifadhi sunnahh na Itikadi na kuipiga vita bida'a na mambo ya batili na mambo ya kuzua.

Ndugu yangu Muislam kwa muda ambao umedumu kufuata mmoja katika maimamu wa madhehebu hayo, hii ndio itikadi ya Imamu wako, kama unavyo mfuata katika hukumu zingine basi mfuate katika Itikadi.

Risala hii imepangiliwa kwa njia ya maswali na majibu ili kurahisisha kupata elimu na kuithibitisha

Tunamuomba Allah atuafikishe wote kuikubali haki na kuwa na Ikhlasi ndani yake na kumfuata Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake

Na rehma na amani za Allah ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad na ali zake na Maswahaba zake.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Nanai Mola wako?

Jawabu/ Sema: Mola wangu ni Mwenyezi Mungu Mwenye kumiliki, Muumbaji, mwenye kupangilia mambo, Anae vipa sura kila viumbe, Mlezi, Mwenye kuvifanyia wema viumbe vyake na kuwasimamia kwa kila jambo, halipatikani jambo lolote ila kwa amri yake na hakuna kinacho tembea ila kwa idhini yake na kutaka kwake.

## Swali/ Utakapo ulizwa ni kwa kitu gani umemjua Mola wako mlez?

Jawabu/ Sema: Nimemjua kwa maumbile ambayo aliyo niumba nayo ya kumjua na kukiri kimaumbile kwa kuwepo yeye Mwenyezi Mungu na kumtukuza na kumuogopa yeye, kama nilivyo mjua kwa kutizama na kuzingatia katika dalili zake na viumbe vyake, kama alivyo sema Allah Mtukufu: {Miongoni mwa dalili zake ni usiku na mchana na jua na mwezi} surat Fuswilat, viumbe hivyo vimeumbwa kwa mpangilio wake na umakini na uzuri haviwezi kujipatisha vyenyewe lazima viwe na muumbaji alie viweka baada ya kuwa havipo na viumbe hivyoni hoja za mkato juu ya kuwepo kwa aliye viumba mwenye uwezo mkubwa na mwenye hekima, viumbe vyote vina kiri kuwepo muumbaji wao na Mfalme wao na mwenye kuwapa rizki na mwenye kuwapangilia mambo ya rizki zako na mambo yao

ispokuwa watu wachache ambao hawa kiri hivyo, Miongoni mwa viumbe vyake: Mbingu saba na Ardhi saba na vilivyomo katia viumbe ambavyo hakuna yeyote anae jua idadi yake na uhakika wake na hali za viumbe hivyo ila ni Allah na hakuna anae vilea na kuviruzuku ila ni Allah aliye hai na mwenyekusimamia mambo yote mwenye uwezo wa kuumba na mwenye sifa ya ukubwa, anasema Allah mtukufu: {Hakika Mola Mlezi wenu ni Mwenyezi Mungu aliye ziumba mbingu na Ardhi katika siku sita. Kisha akatawala juu ya Kiti cha Enzi. Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi. Na jua na mwezi na nyota zinazo tumika kwa amri yake. Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote} Al-A'raaf 54

## Swali/ Utakapo ulizwa ni ipi dini yako?

Jawabu/ Sema: Dini yangu ni Uislam na maana ya Uislam ni kujisalimisha kwa Allah kwa kumpwekesha na kunyenyekea kwake kwa kumtii Allah na kujiweka mbali na Ushirikina na washiriina, kama alivyo sema Allah Mtukufu: (Hakika dini inayo kubaliwa kwa Allah niUislam) Al-Imran 19. na amesema Allah Mtukufu: (Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye akhera atakuwa katika wenye kukhasiri) Al-Imran 85. Mwenyezi Mungu hakubali dini isiyokuwa dini yake ambayo alimtuma Mtume wake Muhammad

rehma na amani za Allah ziwe juu yake, kwa sababu ndio iliyo futa sheria zote zilizo tangulia na yeyote mwenye kufuata dini usio kuwa Uislam huyo atakuwa amepotea njia ya uongofu na akhera atakuwa miongoni mwa watu wenye hasara watakao ingia katika jahanam naubaya ulioje wa mafikio yake

## Swali/ Utakapo ulizwa ni zipi nguzo za Imani?

Jawabu/ Nguzo za imani ni sita nazo: Ni kumuamini Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake na Siku ya mwisho na kuamini Qadar ya Kheri za Allah na Shari zote zinatokana na Mwenyezi Mungu mtukufu

Na haitimii imani ya mtu ispokuwa atakapo amini mambo hayo yoote kwa namna ambayo Qur'an na Sunnahh za Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake zimeelekeza na mwenye kukanusha moja katika hayo atakuwa ametoka katika Uislam na ushahidi wa hayo ni kauliya Allah Mtukufu: {Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri na waombao na katika ukombozi na akawa anashika Sala na akatoa Zaka

na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi na wanao vumilia katika shida na dhiki na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha na hao ndio wajilindao.} (Al-Baqarah 177) na kauli ya Mtumerehma na amani za Allah ziwe juu yake wakati alipo ulizwa kuhusu Imani, alisema: (Ni kumuamini Mwenezi Mungu na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake na Kuamini siku ya mwisho na kuamini Qadar ya Allah ya heri zake na shari zake) Imepokelewa na Imamu Muslim.

## Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kumuamini Mwenezi Mungu Mtukufu?

Jawabu/ Sema: Kumuamini Mwenezi Mungu nikusadikisha na kuwa na yakini na kukiri kuwepo kwa Allah Mtukufu na upweke wake katika Ungu wake na katika ibada zake na katika majina yake na sifa zake.

## Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kumuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu Mtukufu?

Jawabu/ Sema: Ni kusadikisha na kuamini kwa mkato juu ya kuwepo kwa Malaika na sifa zao na uwezo wao na kazi zao na yale wanayo amrishwa, na kwamba wao ni viumbe vya Allah vitukufu vikubwa Allah ameviumba kutokana na Nuru, Amesema Allah Mtukufu: {Hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayo waamrisha na wanatenda

wanayo amrishwa} (Attahriim 6) na wana mbawa mbili na tatu na nne na zaidi ya mbawa hizo na idadi yao ni kubwa mno na hakuna anae jua idadi yao ila ni Allah Mtukufu. Na akawakalifisha Mwenyezi Mungu kwa majukumu makubwa, miongoni mwao kuna walio beba Arshi na kuna walio wakilishwa kwa ajili ya vizazi na kuna wanao hifadhi matendo ya viumbe na kuna wanao hifadhi viumbe na kuna walinzi wa pepo na moto na majukumu mengine na mbora wa malaika ni Jibril -amaniziwe juu yake- na yeye amekalifishwa na kazi ya kushusha wahyi (Ufunuo) kwa Mitume. tunapaswa kuamini kuwepo kwa malaika kwa jumla na kwa upambanuzi kama alivyo tueleza Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kitabu chake na katika sunnahh za Mtume rehma na amani ziwe juu yake na mwenye kukanusha kuwepo kwa malaika au akadai kuwa uhakika wa malaika uko tofauti na alivyo eleza Mwenyezi Mungu Mtukufu basi mtu huyo anakuwa kafiri kwa kukadhibisha kwake habari ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na habari ya Mtume rehma na amaniziwe juu yake.

## Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kuamini vitabu vilivyo shushwa?

Jawabu/ Sema: Ni kuakinisha na kushahidilia kuwa Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ameshusha juu ya manabii wake rehma na amani ziwe juu yao vitabu na ametaja miongoni mwa vitabu hivyo ni:

Kurasa za Ibrahim Tawrati Injili Zaburi na Qur'an, akashusha Kurasa zaIbrahim kwa nabii Ibrahim na Tawrat kwa nabii Musa na Injiri kwa nabii Issa na Zaburi kwa nabii Daud na Qur'an kwa nabi Muhammad Amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote.

Na kitabu bora ni Qur'an ambacho ni maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliyasema kwa hakika wa matamshi yake na maana yake kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na akamsikilizisha Jibril amani ziwe juu yake, kisha akamuamrisha kuyafikisha kwa Mtume Muhammad rehmana na amani ziwe juu yake, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Imeteremshwa na Malaika mwaminifu} (Shuaraa 193) na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Hakika Sisi tumekuteremshia Qur'ani kidogo kidogo} (Al Insan 23) na kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu: {Mpeulinzi apate kusikia maneno ya Mwenyezi Mungu} (Tawba 6).

Na hakika Allah ameihifadhi Qur'an kutokana na kupotoshwa kuzidishwa na kupunguzwa na kitabu hicho kimehifadhiwa katika vitabu na vifua mpaka Mwenyezi Mungu atakapo zichukua roho za waumini kabla ya kusimama kiyama katika zama za mwisho, atakinyanyua kitabu hicho kwake na hakutabaki chochote katika Qur'an.

## Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kumuamini Manabii na Mitume?

Jawabu/ Sema: Ninaamini kwa mkato kwamba Mitume wote ni wanadamu, kwamba wao ni watu wema katika watoto wa Adamu na kwamba Mwenyezi Mungu amewachagua kwa ajili ya kufikisha sheria yake ambayo aliyo iteremsha kwa waja wake, Mitume hao wanawalingania wanadamu wamuabudu Mwenyezi Mungu mmoja ambae hana mshirika na kujiweka mbali na ushirikina na washirikina. na utume ni kuchaguliwa na Mwenyezi Mungu na haupatikani kwa kujitahidi wala kwa kufanya ibada nyingi, wala kwa kuwa mwema au akili nyingi, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Mwenyezi Mungu anajua wapi aweke utume wake} (Al Anaam 124).

Na Nabii wa kwanza ni Adam amani ziwe juu yake, na Mtume wa kwanza ni Nuhu amani ziwe juu yake na Mtume wa mwisho na mbora wao ni Muhammad Bin Abdillah Mkurayshi katika koo ya banii hashim, sala na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote, na mwenye kukanusha Mtume atakuwa amekufuru na mwenye kudai utume baada ya Muhammad rehma na amani ziwe juu yake atakuwa ni kafiri mwenye kumkadhibisha Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu anasema: {Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi

Mungu na Mwisho wa Manabii...} (Al-Ahzab 40), na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Hakuna Mtume baada yangu).

## Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kuamini siku ya mwisho?

Jawabu/ sema: Ninaamini kwa mkato na yakini isiyokowa na shaka ndani yake na nikiwa ni mwenye kukiri kutokea yote aliyo yaeleza Mwenyezi Mungu kuhusu kutokea kwake baada ya kufa, ikiwemo kuulizwa maswali kaburini na neema za kaburini na adhabu zake na kufufuliwa na kukusanywa viumbe kwa ajili ya kuhesabiwa na kuhukumiwa na yale yatakayo kuwa katika uwanja wa kufufuliwa, ikiwemo kisimamo kirefu na jua kusogea kiasi cha maili moja na hawdhwi (Bwawa) na mizani na kupewa vitabu vya matendo ya waja na kuwekwanjia ambayo itakuwa juu ya moto wa Jahanam na mengineyo miongoni mwa matukio na vitisho vya siku hiyo kubwa, mpaka watu wa peponi waingie peponi na watu wa motoni waingie Motoni, kama ilivyo elezwa kwa uwazi katika Qur'an na sunnah za Mtume rehma na amani ziwe juu yake na inaingia katika imani ya kuamini siku ya mwisho, kusadikisha yale yalio thibiti katika alama za Qiyama na alama zake ikiwemo fitina kukithiri, kuuwana , matetemeko na kudidimizwa ardhini,na kutoka Dajali na kushuka kwa nabii Issa amani ziwe juu yake na kutoka kwa Yaajuju na Maajuju na

kuchomoza jua kutoka katika upande wa Magharibi na alama zinginezo miongoni mwa alama za Qiyama.

Na zote hizo zimethibiti katika kitabu cha Mwenyezi Mungu na habari za Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake zilizo sahihi zilizo andikwa katika vitabu vya Hadithi sahihi.

## Swali/ Utakapo Ulizwa: Je Adhabu za kaburi na neema zake zimethibiti katika Qur'an na sunnah?

Jawabu/ Sema: Ndio, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: {Wanaonyeshwa Moto asubuhi na jioni. Na itapo fika Saa ya Qiyama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!} (Ghafir 46), na amesema Mwenyezi Mungu: {Na laiti ungeli ona Malaika wanapo wafisha wale walio kufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao na kuwaambia: Ionjeni adhabu ya Moto!} (Anfal 50), na kauli ya Mwenyezi Mungu: {Mwenyezi Mungu huwatia imara wenye kuamini kwa kauli ya imara katika maisha ya dunia na katika akhera} (Ibrahim 27) na imekuja katika hadithi Qudsiy ndefu kutoka kwa swahaba Baraa -radhi za Allah ziwe juu yake-: (Atanadi mwenye kunadi mbinguni akisema: Amesema ukweli mjawangu mtandikieni peponi na mumvishe mavazi ya watu wa peponi na mfungulieni mlango wa pepo,

inatoka katika pepo hiyo harufu nzuri kisha kaburi lake linapanuliwa, inakuwa kubwa kiasi cha upeo wa macho yake na hakika kafiri, kisha akataja hali anayo ipata wakati wa kufa kwake, akasema: Kisha roho yake inarejeshwa katika mwili wake, kisha wanamjia Malaika wawili, kisha wanamkalisha, kisha wanamuuliza: Nani mola wako? atajibu: haa haa sijuwi, kisha wanamuuliza ni ipi dini yako? atajibu haa haa sijuwi, kisha watamuuliza niyupi huyo mwanaume alie tumwa kwenu? atajibu: haa haa sijuwi, atanadi mwenye kunadi mbinguni akisema: huyo amesema uwongo mtandikieni matandiko ya motoni na mvisheni mavazi ya watu wa motoni na mfungulieni mlango wa moto, kisha ule moto na joto na sumu zake vinamjia, kisha kaburi linambana mpaka mbavu zake zinatofautiana. Amezidisha mpokezi katika riwaya: (Kisha analetewa malaika asie ona wala hazungumzi, akiwa na nyundo kubwa na nzito ya chuma, laiti ungepigwa mlima kwa nyundo hiyo mlima ungesagika ukawa kama mchanga, kisha anapigwa nayo pigo moja ambalo viumbe vyote vya mashariki namagharibi vinasikia ila watu na majini hawasikii). Imepokelewa na Abudaud. Kwa sababu ya jambo hili ndio maana Mtume akatuamrisha tujilinde kwake na adhabu za kaburini katika kila swala.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Hivi waumini watamuona mola wao siku ya Qiyama?

Jawabu/ Sema: ndio watamuona mola wao siku ya Akhera na miongoni mwa dalili juu ya hilo ni kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu: {Nyuso za watu siku ya Qiyama zitakuwa na nuru (22) zikimuangalia mola wao mlezi} alqiyama (22-23) na kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, (Hakika nyinyi mtamuona mola wenu) imetolewa na Imamu Bukhari na Muslim, na zimekuja hadithi zilizo sahihi kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika kuthibitisha kuwa waumini watamuona Mola wao Mtukufu na maswahaba wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake wamekubaliana juu ya hilo na Mataabii na walio wafuata kwa wema. Atakae kanusha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu atakuwa amemfanyia uadui Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake na atakuwa amekhalifu njia ya waislamkuanzia maswahaba wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake na walio wafuata kwa wema. Ama Mwenyezi Mungu kuonekana Duniani haiwezekani kuonekana kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ( Hakika nyinyi hamta muona mola wenu mpaka mtakapo kufa) na nabii Mussa -amani ziwe juu yake-zama alipo muomba Mwenyezi Mungu amuone duniani kama ilivyo kuja katika kauli ya Mwenyezi Mungu: {Na alipokuja Mussa kwa wakati uliowekwa na

Akasema na yeye Mola, alisema Mussa Mola wangu naomba nikuone, akamjibu Mwenyezi MunguAkamwambia, Hutoniona} (Al-Aaraf 143).

## Swali/ Utakapo ulizwa: Kuamini Hukumu ya Mwenyezi Mungu na Qadar zake inakuwa vipi?

Jawabu/ Sema: Inakuwa kwa yakini ya mkato kwamba kila kitu kinakuwa kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu na mipangilio yake, hakiwi kitu chochote ila kwa utashi wake, yeye ndie alie umba vitendo vya waja wake vya heri na shari, na akawaumba waja wake katika maumbile ya heri na ya kukubali haki, na akawapa akili yenye kupambanua na akawaruzuku utashi ambao watachagua wanacho kipenda kwa utashi huo, na akawabainishia haki na akawatahadhalisha na batili, akamuongoza anae mtaka kwa fadhila zake na akampoteza anae mtaka kwa uadilifu wake, yeye ndie mwenye hekima na ni mjuzi mwenye huruma, haulizwi kwa anacho kifanya na waja wanaulizwa kwa kila wanacho kifanya.

Daraja za Qadar ni nne:

Daraja ya kwanza: Ni kuamini elimu ya Mwenyezi Mungu kwamba yeye amekizunguka kila kitu, yeye ni mjuzi kwa yale yalio tokea na yale yanayo tokea na yale ambayo hayajatokea, kama yangetokea yangekua vipi.

Daraja la pili: Ni kuamini kwamba Mwenyezi Mungu aliandika kila kitu.

Daraja la tatu: Ni kuamini kwamba kwa Mwenyezi Mungu hakiwi chochote ila kwa utashi wake.

Daraja la nne: Ni kuamini kwamba Mwenyezi Mungu ndie alie umba kila kitu, yeye ndie alie umba dhati ya vitu na matendo na maneno na harakati na utulivu na sifa na kila kitu katika ulimwengu wa juu na wachini na wa aridhini, na dalili za yalio tangulia ziku nyingi katika kitabu cha Mwenyezi Mungu na suna za Mtume.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Mwanadamu anaendeshwa katika mambo yote anayo yafanya au amekhiyarishwa?

Jawabu/ Sema: Haisemwi kuwa Mwanadamu anaendeshwa katika mambo yote au amekhiyarishwa yote mawili ni makosa, dalili za kitabu na sunnahh zimeonyesha kuwa mwanadamu ana utashi wake na kwamba yeye ndie mtendaji kwa uhakika wake, lakini yote hayo hayatoki katika elimu ya Mwenyezi Mungu utashi wake, kinacho bainisha hayo ni kauli ya mwenyezi Mungu: {Kwa mwenyekutaka miongoni mwenu, kulingana na kushikamana juu ya haki na Imani (28) Wala nyinyi hamtotaka isipokuwa kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote} (Takwiir

28-29) na amesema Mwenyezi Mungu: {Mwenye kutaka ataizingatia (55) na hawata zingatia na kuwaidhika ila akitaka Mwenyezi Mungu yeye ndie anae stahiki kuogopwa na yeye ndie anaestahiki kusamehe} (Mudathir 55-56)

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Inaswihi imani bila Matendo?

Jawabu/ sema: Haiswihi imani bila matendo bali matendo ni lazima kwasababu matendo ni nguzo katika imani, ilivyo tamkwa na wanachuoni nikwamba ninguzo katika Imani, na wanachuoni wamekubaliana katika hilo kwamba imani ni kauli na vitendo na ushahidi juu ya hilo ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na atakae kuendea MwenyeziMungu akiwa amefanya matendo mema hao ndio wenye daraja la juu} tah 75, Mwenyezi Mungu akaweka sharti la imani na matendo pamoja ili mtu aingie peponi.

## Swali/ Utakapo ulizwa ni zipi nguzo za Uislam?

Jawabu/ Sema: ni Tano, nazo: Ni kushahidilia kuwa hapana mungu apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mungu mmoja na kwamba Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na kusimamisha swala na kufunga ramadhani na kutoa zaka nakuhiji katika nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu.

Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Uislam umejengewa juu ya mambo matano: Ni kushahidilia kuwa hapana mungu apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mungu mmoja na kwamba muhammad ni mtume wa Mwenyezi Mungu na kusimamisha swala na kutoa zaka na kuhiji katika nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu na kufunga Ramadhani) Imepokelewa na Bukhari na Muslim.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi maana ya shahada kuwa hapana Mungu apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mungu mmoja na kwamba Muhammad nimtume wa Mwenyezi Mungu?

Jawabu/ sema: Shahada kuwa hapana Mungu apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu: Maana yake: Hakuna wa kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu kama ilivyo katika kauli ya Mwenyezi Mungu: {Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayo yaabudu. (26) Isipo kuwa yule aliye niumba, kwani Yeye ataniongoa. (27) Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee}. (Zukhruf 26-28) na amesema Mwenyezi Mungu:{ Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu huuingiza usiku katika mchana na huuingiza mchana katika usiku na amedhalilisha jua na mwezi? Vyote hivyo

vinakwenda mpaka wakati ulio wekwa. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayo yatenda}. (Luqman 29).

Na maana ya Shahada ya kuwa muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu: Ni kuyakinisha yakwamba ni mja wa Mwenyezi Mungu na nimtume wake na kwamba yeye ni mtumwa haabudiwi na ni mtume hakadhibishwi, anatiiwa kwa yale aliyo yaamrisha na anasadikishwa kwa yale aliyo yaeleza na yanatengwa mbali yale yote aliyo yakataza na kuyakemeya na asiabudiwe Mwenyezi Mungu ila kwa sheria yake bila kuzidisha wala kupunguza.

Na haki ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake juu ya Ummah wake, ni kumuheshimu na kumtukuza na kumpenda na kumfuata, katika kila wakati na zama kwa kadri ya uwezo, amesema Mwenyezi Mungu: {Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu.} (Al Imran 31).

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni yapi masharti ya Lailaha ila Allah?

Jawabu/ Sema: Neno la tawhiid halitoshi kutamkwa bila ya kuitakidi na kuzingatia na kusimamia mambo yanayo pelekea kutamka neno hilo na kujiepusha na mambo yanayo yatengua,

bali neno hilo lina masharti saba, wanachuoni wameyatoa masharti hayo katika dalili ya kisheria, wakaziandika na kuzitolea dalili katika Qur'an na Sunnah nazo:

1- Elimu kwa maana yake katika kukanusha na kuthibitisha, ni kujua kuwa hakika Mwenyezi Mungu hana mshirika na yeye ndie anaestahiki kuabudiwa na dalili ambazo zimeonyesha kukanusha Uungu kwa asiekuwa Mwenyezi Mungu na kujua mambo ya lazima na yanayo takiwa kufanywa baada ya kutamka neno hilo pia nakujua mambo yanayo batilisha neno hilo, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: {Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu} (muhammad 19) na amesema Mwenyezi Mungu: {Isipo kuwa anaye shuhudia kwa haki na waowanajua} (Zukhruf 86), amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Atakae kufa akiwa anajua kuwa hakuna Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Allah ataingia peponi) Imepokelewa na Imamu muslim.

2- Yakini nayo: nikuitakidi kwa mkato juu ya neno hilo la shahada, yakini ambayo inayo pingana na Shaka au wasiwasi, yakini ilio thibiti katika moyo, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Hakika Waumini ni wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tenawasitie shaka kabisa na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio wakweli}(Al-

Hujrat 15) na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Atakae sema ninashahidilia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila niMwenyezi Mungu na mimi ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu mja hakutani na Mwenyezi Mungu akiwa na shahada hizo mbili bila ya kuwa na mashaka katika hizo shahada ila ataingia peponi) Imepokelewa na Muslim.

3- Ikhlasi inayo pinga Ushirikina, kwasababu ya kusafisha Ibada na kuitakatisha kutokana na uchafu wa ushirikina, au kujionyesha. Amesema Allah mtukufu: {Hakika dini Safi ni ya Mwenyezi Mungu tu}. (Zumar 3) na amesema Allah mtukufu: {Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia dini} (Albayyinah 5) na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ( Watu watakao pata mafanikio ya uombezi wangu siku ya Qiyama, ni mtu aliesema Lailaha ila Allah akiwa na Ikhlas katika moyo wake na nafsi yake) Imepokelewa na Imamu Bukhary.

4- Mapenzi (Mahaba) ya neno hilo la tawhiid na yale ambayo yanayo elezwa na neno hilo, na kufurahia hilo, na kuwapenda wenye kulisema neno hilo, na kukithirisha mapenzi kwao, na kuwachukia wanao lipinga neno hilo na kujitenga mbali nao wakiwemo makafiri, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:,{Na katika watu wapo wanao chukua waungu wasio kuwa Mwenyezi

Mungu. Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walio amini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana} (Al-Baqara 165) na amesema Mtume rehma na amani ziwe juuyake: (Mambo matatu atakae kuwa nayo atapata utamu wa imani, awe Allah na Mtume wake ndio vipenzi vyake kuliko vitu vyote, na ampende mtu hampendi kwa lolote ila ni kwa ajili ya Allah, na achukie kurudi katika ukafiri kama anavyo chukia kutupwa Motoni) Imepokelewa na Imamu Muslim.

5- Ukweli unao pingana na Uwongo na ukweli unakuwa kwa Moyo kuafikiana na viungo katika kile kilicho tamkwa na ulimi ambacho ni neno la Tawhiid, viungo vinasadikisha moyo kwa maneno yaliyo semwa na moyo huo vinafanya Ibada za wazi na za ndani, Amesema Allah mtukufu: {Mwenyezi Mungu atawatambulisha walio wa kweli na atawatambulisha walio waongo} (Al-Ankabuti 3) na amesema Allah Mtukufu: {Na aliye ileta Kweli na akaithibitisha - hao ndio wacha Mungu} (Azzumar 33) na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Atakae kufa akiwa anashahidilia kuwa Hapana Mungu apasae kuabudiwa kwa haki na Muhammad ni mtume wa Allah akiwa ni mkweli katika moyo wake ataingia peponi) Imepokelewa na Imamu Ahmad.

6- Kuzingatia, kwa kunyenyekea kwa ajili ya Allah kwa kumpwekesha katika ibada na kuleta haki zake

kwa kutekeleza maamrisho yake nakujiepusha na makatazo yake kwa Ikhlasi kutaka thawabu na kutarajia malipo kwa Allah na kwa kumuogopa Allah, Amesema Allah mtukufu: {Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi na silimuni kwake} (Zumar 54), na amesema Allah Mtukufu {Na mwenye kuuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu naye akawa anafanya wema, basi huyo hakika amekwisha kamata fundo lilio madhubuti} (Luqman 22).

7- Kukubali kunako pingana na kukataa na inakuwa kwa moyo kukubali neno la tawhiid na yale yanayo patikana katika tamko hilo, lakini neno hilo halipokelewi kwa mwenye kujidai kufuata neno hilo kwa kujibaguwa na wengine au kwa kiburi, Anasema Allah mtukufu :{Wao walipo kuwa wakiambiwa La ilaha illa 'Llahu Hapana mungu ila Mwenyezi Mungu tu, wakijivuna} (Swafati 35). Huyo hawi Muislamu.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Nani Mtume wako?

Jawabu/ Sema: Ni muhammad Bin Abillah Bin AbdilMutwalib Bin Hashim Bin Abdilmanafi. Mwenyezi Mungu alimchagua kutoka katika kabila la kiqurayshi nao ni Watoto wa Ismaili Bin Ibrahim Amani ziwe juu yao, Mwenyezi Mungu alimtuma kwa majini na watu na akamshushia kitabu na

hekima na akamfanya ni mtume bora na ni mbora wa Mitume rehma na amani ziwe juu yake.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni kipi cha kwanza alicho faradhisha Mwenyezi Mungu kwa waja wake?

Jawabu/ Sema: Ibada ya kwanza aliyo ifaradhisha ni Imani ya kumuamini yeye Mwenzi Mungu Mtukufu na kukufuru vyote visivyokuwa yeye (Twaghuti), kama alivyo sema: {Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu na muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo alio waongoa MwenyeziMungu. Na kati yao wapo ambao ulio wathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanao kanusha} ( Annahli 36) Na Twaghuti: Ni kila jambo ambalo mja amechupa mipaka katika katika kinacho fuatwa au kuabudiwa au kutiiwa.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Mwenyezi Mungu ameumba viumbe kwa sababu gani?

Jawabu/ Sema: Amebainisha Allah ukweli wa kubainisha malengo hayo, kwamba aliumba viumbe watu na majini ili wamuabudu yeye peke yake hana mshirika na ibada hiyo ni kutii amri zake na nikujiepkusha na makatazo yake, Amesema Allah Mtukufu: {Nami sikuwaumbamajini na watu ila waniabudu Mimi} (Adh- dhariyat 56) na

amesema Allah Mtukufu: {Muabuduni Mwenyezi Mungu na msimshirikishe na chochote} (Annisaa 36).

## Swali/ Ukiulizwa: Nini maana ya Ibada?

Jawabu/ Sema: Ibada ni kila anacho penda Allah na kukiridhia katika Maneno na vitendo vya ndani na nje, ambavyo ametuamrisha Allah Mtukufu kuviamini au kuvisema au kuvifanya, kama kumuogopa yeye kumtaraji, bkumpenda, kumuomba msaada, kumuomba nusra na kuswali na kufunga.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Dua ni katika Ibada?

Jawabu/ Sema: Hakika Dua ni katika aina kubwa ya ibada, kama alivyo sema Allah mtukufu: {Na Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni. Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike} (Ghafir 60) na katika hadithi : Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Dua ndio Ibada) Imepokelewa na Imamu Tirmidhiy na kwa ukubwa wa dua na umuhimu wake katika dini imekuja dua katika zaidi ya aya mia tatu (300) katika Qur'an Tukufu na dua ina aina mbili:dua ya ibada na dua yaMaombi na kila kimoja hakitimii mpaka kiwe na mwenzake.

Dua ya ibada: Ni kujikurubisha kwa Allah mtukufu kwa ajili ya kupata unacho kitafuta, au kuzuia mabaya, au kuondoa madhara kwa kufanya ikhlas katika ibada za Allah mtukufu. Anasema Allah Mtukufu: {Na Dhun-Nun alipoondoka hali ameghadhibika na akadhani yakwamba hatutakuwa na uwezo juu yake. Basi aliita katika giza: Hapana mungu isipo kuwa Wewe Subhanaka Uliye takasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu (87) Basi tukamwitikia na tukamwokoa kutokana na dhiki. Na hivyo ndivyo tunavyo waokoa Waumini} (Al-Anbiyaa 87-88).

Dua ya Maombi: ni kuomba mambo yenye manufaa kwa muombaji miongoni mwa kuleta manufaa, au kuondoa madhara. Amesema Allah Mtukufu: {Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumeamini, basi tufutie madhambi yetu na tuepushe na adhabu ya Moto} (Al-Imran 16)

Dua kwa aina zake mbili ndio ubongo wa ibada kwa uchache wake nayo ni ibada nyepesi kwa kuiomba na ndiyo yenye cheo cha juu na athari kubwa, dua ni sababu yenye nguvu katika kuzuia mambo mabaya na mtu kupata kile anacho kitafuta kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

## Swali/ utakapo ulizwa: ni yapi masharti ya kukubaliwa ibada kwa Allah Mtukufu?

Jawabu/ Sema: Ibada haikubaliwi kwa Allah mpaka itimize masharti mawili: Sharti la kwanza: Ibada iwe kwa ajili ya Allah mtukufu na ushahidi ni Kauli yake Mwenyezi Mungu: {Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia dini} (Albayyinah 5) na amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: {Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi} (Kahfi 110)

Sharti la pili: Iwe ibada ni yenye kuafikiana na sheria aliyo kujanayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake na dalili ni kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu: {Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu} (Al-Imran31). na kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenyekufanya ibada ambayo haipo katika dini yetu basi atarudishia mwenyewe) Imepokelewa na Imamu Muslim. na kama ibada haikubaliani na uongofu wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakika ibada hiyo haikubaliwi hatakama alie ifanya ameifanya kwa ajili ya Allah.

## Swali/ Utakapo Ulizwa: Je, inajuzu kuwa na imani njema bila ya matendo?

Jawabu/ Sema: Hapana, lazima vikusanyike na Nia safi ambayo ni kufanya Ibada kwa ajili ya Allah na yenye kuafikiana na sheria ya Mtume wa Allah rehma na amani ziwe juu yake. Dalili ya hayo ni Kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu: {Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi} (Kahfi 110). Mwenyezi Mungu mtukufu akaweka sharti katika aya hii kwamba ili matendo yawe mema lazima iwe kuna nia njema na yawe matendo yako ni memana yenye kukubaliana na sheria ya Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni zipi aina za Tawhiid?

Jawabu/ Sema: Tawhiidi ina vigawanyo vitatu:

1. Tawhiid Rububiyyah: nayo ni kuitakidi kwa mkato kwamba Mwenyezi Mungu ndie muumbaji anae toa rizki na mwenye kupangikia mambo ya waja wake wote, hana Mshirika wala msaidizi na yo ni kumkwekesa Mwenyezi Mungukwa vitendo vyake Allah, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Ati yupo muumba mwengine asiye kuwa Mwenyezi Mungu anaye kupeni riziki kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Hapana mungu ila

Yeye tu. Basi wapi mnako geuzwa?} (Fatwir 3) na anasema Mwenyezi Mungu: {Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu, Madhubuti}. (adh-adhariyat 58) na anasema Mwenyezi Mungu: {Anapitisha mambo yote yalio baina mbingu na ardhi} (Asajidah 5) na amesema Mwenyezi Mungu: {Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote} (Al-Aaraf 54).

2- Tawhiidul Asmaai wa swifati: nayo ni kuitakidi kwamba Mwenyezi Mungu ana majina mazuri na sifa zilizo kamilika zilizo thibiti katika Qur'an na Sunnahh, bila kufananisha wala kulinganisha, wala kupindisha wala kugeuza na kwamba Mwenyezi Mungu hana mfanowa kitu chochote, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: { Hana mfano wa chochote na yeye nimsikivu na anaona} (Shura 11). na amesema Mwenyezi Mungu: {Mwenyezi Mungu ana majina mazuri muombeni kupitia majina hayo} (Surat Al-Ar'raf 180).

3- Tawhiid Al-Uluhiyyah: nayo ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu pekeyake hana mshirika katika ibada, yaani kumpwekwsha Mwenyezi Mungu katika vitendo vya waja wake inaitwa tawhiidi ya kiibada, amesema Mwenyezi Mungu: {Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia dini} (Albayyinah 5) na amesema Mwenyezi Mungu: { Na hatukumtuma

kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu} (Al-Anbiyaai 25) na mgawanyo huu ni kwajili ya kuweka wazi maswala ya kielimu na kama sio hivyo huo mgawanyo unalazima kuwepo katika itikadi ya kila Muislam mwenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu na mwnye kufuata Kitabu na sunnahh.

## Swali/ Utakapo ulizwa ni ipi dhambi kubwa ambayo aliasiwa Mwenyezi Mungu kwayo?

Jawabu/ Sema: Ni Ushirikina amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Hakika wamekufuru walio sema: Mwenyezi Mungu ni Masihi mwana wa Maryamu! Na hali Masihi mwenyewe alisema: Enyi Wana wa Israili! Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharamishia Pepo na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru} (Al-Maida 72) na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi kushirikishwa na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye} (Annisaa 48) kitendo cha kuwa Mwenyezi Mungu hasamehi dhambi za Mshirikina akifa hajatubia ni alama kuwa Shirki ni dhambi kubwa, kinacho bainisha hilo ni kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake

pindi alipo ulizwa: ni ipi dhambi kubwa? akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (ni kumfanya Mwenyezi Mungu kuwa ana msaidizi wake au mfano wake katika viumbe ilihali yeye amekuumba...) Imepokelewa na Bukhari na Muslim.

Ushirikina: Ni Mtu kumjalia Mwenyezi Mungu kuwa na msaidizi wake ambae wako sawa katika kazi zake au anayo sifa miongoni mwa sifa zake, katika Malaika au Mtume au Walii namfano wake, anaamini kuwepo chochote kwa kiumbe huyo katika sifa za Mwenyezi Mungu na mambo yanayo Muhusu yeye ikiwemo kuumba au ufalme au kupangikia mambo yoote ya wajawake, au akajikurubisha kwake akawa anamuomba, au kumtarajia, au kumuogopa, au anategemea, au anataka kwake kinyume cha Mwenyezi Mungu au pamoja na Mwenyezi Mungu, akakifanyia chochote katika aina za ibada za mali au mwili za dhahiri au zilizo jificha.

## Swali/ Utakapo ulizwa ni vingapi vigawanyo vya Ushirikina?

Jawabu/ Sema: Ushirikina umegawanyika mara mbili:

1- Shirki Kubwa: Nayo ni kukifanyia ibada kisichokuwa Mwenyezi Mungu, Kama kutegemea kwa asiekuwa Mwenyezi Mungu, au kuomba

msaada kwa walio kufa, au kukichinjia kisichokuwa Mwenyezi Mungu, au kutoa nadhiri kwa kisichokuwa Mwenyezi Mungu, au kukisujudia kisichokuwa Mwenyezi Mungu, au kuomba nusra kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika mambo ambayo hakuna mwenye uwezo nayo ila ni Mwenyezi Mungu, kama kuomba nusra kwa wasio kuwepo, au walio kufa na hakuna anaefanya mambo haya ya kijinga ila mwenye kuitakidi uwezo wao wa kujibu na kwamba wana uwezo wa kufanya mambo ambayo hakuna mja anaweza kufanya ila ni Mwwnyezi Mungu, anakuwa kwa kitendo hicho ameitakidi kwa kiumbe huyo kuwa na mambo yanayo muhusu Mwenyezi Mungu, anakinyenyekea na kujidhalilisha kwake udhalili wa kukiabudu na anakitegemea katika mambo yake na anaomba nusra kwa kitu hicho na anakiita akiomba mambo ambayo hakuna kiumbe anaeweza kumtimizia. Na jambo la ajabu ni mtu kuomba nusra kwa kitu ambacho hakina uwezo wowote hakimiliki kujiletea manufaa wala kujikinga na Madhara, hakimiliki kifo wala uhai wala kufufuliwa na mtu ambae hawezi kujiletea manufaa wala kuzuia madhara juu ya nafsi yake vipi atamiliki vitu hivyo kwa watu wengine, kitendo hiki ni kama mfano wa mtu anae zama baharini kumuomba msaadamwenzake ambae anazama.Utakasifu ni wa Mwenyezi Mungu! Vipi yamefunga macho ya washirikina na kuondoka kwa akili zao wakadiriki

kufanya Ushirikina unaopingana na sheria ya Mwenyezi Mungu, Ushirikina unao pingana na akili salama, pia Ushirikina unao pingana na Maumbile!

2- Shirki ndogo: Mfano wa kujionyesha kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Jambo kubwa ambalo ninalo chelea kwenu ni Shirki ndogo, akaulizwa kuhusu shirki ndogo akasema: Kujionyesha (Riyaa) Imepokelewa na Muslim na mfano mwingine wa shirkindogo ni kuapia kwa kisichokuwa Mwenyezi Mungu, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenyekuapia kisichokuwa Mwenyezi Mungu atakuwa amekufuru au amefanya shirki) Imepokelewa na Tirmidhy.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni zipi aina za Ukafiri?

Jawabu/ Sema: Ukafiri upo aina mbili:

1- Ukafiri mkubwa: unamtoa mtu katika uislam nao ni wenye kupingana na uislam kama mwenye kumtukana Allah au mtume wake au dini yake au akafanya masihara au istihzai katika sheria ya uislam au akaikataa habari ya Allah au amri yake au makatazo yake, akakadhibisha yale aliyoyaeleza Allah na mtume wake au akakanusha chochote alicho kifaradhisha Allah kwa waja wake, Au akahalalisha aliyoharamisha Allah na mtume wake. Amesema Allah mtukufu: (Sema: Mlikuwa

mkimfanyia masihara Mwenyezi Mungu na ishara zake na Mtume wake? (65) Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu! Tukilisamehe kundi moja kati yenu, tutaliadhibu kundi jingine kwa kuwa wao ni wakosefu) (Tauba 65-66.)

2- Ukafiri mdogo nao ni ule ambao dalili za kisheria zimeuita ni ukafiri na sio ukafiri mkubwa kwa jina jingine unaitwa kukufuru neema au ukafiri mdogo, kama vile muislamu kupigana na muislamu mwenzake, kujivua unasabu na kuomboleza na mfano wake katika mambo ya kijinga amesema mtume rehma na amani ziwe juu yake (kumtukana muislamu ni uovu na kupigana naye ni ukafiri) Imepokelewa na Bukhar, amesema mtume rehma na amani ziwe juu yake: (watu wa aina mbili katika watu wana ukafiri: mwenye kutia dosari kwa nasabu na kuomboleza kwa maiti), imepokelewa na Muslim: Ibada hizi hazimtoi mtu katika Uislamu lakini ni katika madhambi makubwa Allah atuepushe.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni zipi aina za Unafiki?

Jawabu/ Sema: Unafiki upo aina mbili, Unafiki mkubwa na unafiki mdogo.

Unafiki mkubwa: ni kudhihirisha Uislam na kuficha ukafiri na hizi ni katika hathari zake kubwa

kuuchukia uislam na kuuchukia ushindi wake na kuwachukia waislam na kufanya bidii ya kuwapiga vita na kuharibu dini yao.

Unafiki mdogo ni kujifananisha na vitendo vya wanafiki bila kuficha ukafiri, kama mfano anayesema uwongo anapoongea na anapo ahidi hatimizi na anapo aminiwa anafanya hiyana, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake (Alama za mnafiki ni tatu, Akiongea anasema uongo, akiaminiwa anafanya hiyana na anapo ahidi hatimizi)Imepokelewa na Imamu Bukhar.

## Swali/ Utakapo ulizwa ni vitu gani vinavyo tengua Uislam?

Jawabu/ sema: Chenye kutengua maana yake ni chenye kubatilisha na chenye kuharibu, Wakati wowote kinapotokea kwenye jambo uharibu, kama vile vibatilisho vya udhu ambavyo mwenye kuvifanya vinambatilisha udhu na analazimika kutawadha tena, mfano wake ni mfano vinavyobatilisha uislamu, mja anapovifanya uislam wake unaharibika na kubatilika na mtendaji anatoka katika uislamu na kuwa kafiri na wana wa chuoni wametaja katika mlango wa kuritadi na hukmu za mwenye kuritadi wametaja aina nyingi za vitu ambavyo vinaweza kumfanya Muislamu akaritadi na kutoka katika dini yake ikawa halali damu yake na mali yake na vitu vyenye hatari zaidi

na vikubwa na nivingi kwa kutokea na vile ambavyo wanakubaliana wana wa chuoni kuwa vinatengua, ni vitenguzi kumi navyo:

1. Kumshirikisha Allah katika Ibada amesema Allah mtukufu: (Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi kushirikishwa na kitu. Lakini Yeye husamehe yasiyo kuwa hayo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu basi huyo amepotea upotovu wa mbali) (Annisaa 116). Na amesemaAllah mtukufu {Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo na mahala pake ni Motoni. Walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru} (Almaida 72), miongoni mwa kumshirikisha mwenyezi Mungu katika Ibada ni kuviomba visivyo kuwa Allah na kuviomba nusra na kujikinga kwavyo na kuweka nadhiri na kuvichinjia, kama anayemchinja jini au kaburi au walii akiwa hai au hakuwa maiti kwa lengo la kuleta manufaa au kuzuia shari kama wanavyofanya wajinga wanaidanganywa kwa uongo na shubha za waganga waongo na watu wa mazingara.

2. Mwenye kujalia baina yake na baina ua Allah wasaidizi akiwaomba kupona na kumtegemea katika kupata matakwa yake na wanawategemea katika kupata mahitaji yake ya kidunia na ya akhera, mtu huyo itakuwa amekufuru kwa makubaliano ya wana wa chuoni ,amesemaAllah

mtukufu): (sema hakika mimi ninamuomba mola wangu na simshirikishi na chochote) (Al Jinni 20).

3. Mtu ambae hakukufurisha washirikina au akatilia shaka katika ukafiri wao, au akasahihisha madhehebu yao ya ukafiri. Amesema Allah Mtukufu: {Na Mayahudi wanasema: Uzeir ni mwana wa Mungu. Na Wakristo wanasema: Masihi ni mwana wa Mungu. Hiyo ndiyo kauliyao kwa vinywa vyao. Wanayaiga maneno ya walio kufuru kabla yao. Mwenyezi Mungu awaangamize! Wanageuzwa namna gani hawa!} (Tawba 30) kwasababu kuridhia ukafiri ni ukafiri na dini haiswihi dini ispokuwa kwa kukufuru vyote vinavyo abudiwa kinyume cha Allah.(Twaghuti) na kuitakidi ubatili wa dini zote zisizokuwa uislam na kuzichukia na kujitakasa kutokana na dini hizo na wafuasi wa hizo dini na kupigana nao kwa kadri ya uwezavyo.

4. Mwenye kuitakidi kwamba uongofu usiokuwa wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ndio ulio kamilika kuliko uongofu wake, au akaitakidi kwamba hukumu ya asiyekuwa mtume ndio nzuri kuliko hukumu yake, Kama mfano wa yule anae fadhilisha hukumu za Matwaghuti na sheria za viumbe kuwa ndio bora kuliko sheria za Allah na Mtume wake, amesema Allah Mtukufu: {La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo hitalafiana, kisha wasione uzito katika

nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa na wanyenyekee kabisa} (Nisaai 65). Mwenye kutanguliza kauli za Mashekh wa upotevu na mambo yao ya kizushi juu ya sunnahh za Mtume zilizo sahihi akiwa anajua akiwa anajua kuwa hizo sunnahh zimethibiti kuwa ni zamtume, Mwenyekufanya hivyo atakuwa ni kafiri kwa ijimai ya wanachuoni.

5. Mwenye kuchukia chochote katika mambo aliyo kuja nayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake, Hatakama atayafanyia kazi, akiyachukia atakuwa amekufuru, Amesema Allah mtukufu: {Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao}. (Muhammad 9.(

6. Mwenye kufanya masihara na dini aliyo kuja nayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kama mwenye kufanya mzaha na baadhi ya sheria zake na hukumu zake na sunnahh zake na yale aliyo yaeleza, au anafanya masihara na yale aliyo yaeleza Mtume katika malipoya waja watakao fanya mema, au adhabu kwa wenye kufanya Maasi katika yale aliyo yaeleza Mtume rehma na amani ziwe juu yake, mwenye kufanya masihara na hayo yalio tajwa atakuwa amekufuru na ushahidi ni Kauli ya Allah Mtukufu: {(Sema: Mlikuwa mkimfanyia masihara Mwenyezi Mungu na ishara zake na Mtume wake? Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru

baada ya kuamini kwenu! Tukilisamehe kundi moja kati yenu, tutaliadhibu kundi jingine kwa kuwa wao ni wakosefu) } (Tawba 65-66).

7- Uchawi na hauwi ila kwa kutumia majini na mashetani na kuwashirikisha na kufanya mambo ambayo ni yaukafiri, kwa sababu ya kupata radhi zao, miongoni mwa uchawi nikufanya jambo la ajabu lenye kuathiri hisia za watu mwenye kufanya mamno hayo au akaridhiaatakuwa amekufuru na ushahidi ni kauli ya Allah Mtukufu: {Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru}. ( Al Baqara 102).

8- Ni kujumuika na washirikina na kuwasaidia ili wawashinde waislam na dalili ni kauli ya Allah Mtukufu {Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu} (Al Maidah 51).

9- Mwenye kuitakidi kwamba baadhi ya waislam wanaruhusiwa kutoka katika sheria ya Muhammad rehma na amani ziwe juu yake kama Hidhri alivyo toka katika baadhi ya sheria ya nabii Musa rehma ziwe juu yake, mwenye kuitakidi hivyo atakuwa kafiri. dalili ni kauli ya Allah Mtukufu: {Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa

kwake. Naye akhera atakuwa katika wenye hasara}. (Al Imran 85)

10- Ni kuipuuzia dini ya Allah hajifunzi dini wala kuyafanyia kazi maamrisho yake na dalili ni kauli ya Allah Mtukufu: {Na ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye kumbushwa kwa Ishara za Mola wake Mlezi, kisha akazikataa? hakika Sisi tutajilipiza kwa wakosefu} (Sajdah 22). na maana ya kuipuuzia Dini: ni kuto kujifundisha yale yanayo paswa kuyajua katika dini katika yale ambayo ni wajibu katika dini kama kujifunza misingi ya dini kama itikadi na ibada.

Baada ya kutaja hayo ambayo yanabatilisha uislam inapendeze tukawazindua watu kuhusu mambo mawili muhimu nayo:

1. Ni kwamba lengo la kutaja hivi vitenguzi nikutaka kuwakumbusha watu na kuwatahadharisha, hakika shetani na wasaidizi wake miongoni mwa watu wanao potosha dini na kuigeuza wanasubiri mapungufu kwa Waislamu ili watumie nafasi ya kughafilika kwao na ujinga wao ili wawatoe katika Dini ya haki na ili wawatowe katika njia ya pepo na kuwaelekeza kunako njia ya Motoni.

2. Hivi vitenguzi vya uislam kuambatanisha na hali ya kimaisha ili kumpa hukumu kwamba huyu ni kafiri au sio kafiri ni katika majukumu ya wanachuoni wakubwa walio zama katika elimu,

wao ndio wanao jua dalili na hukumu na sababu na vigezo vya kushuka hukumu mbalimbali kwa watu na sio kwa kila mtu anaweza kutoa hukumu hiyo.

## Swali/ Ukiulizwa: inajuzu kumuhukumu mtu duniani kuwa ni mtu wa motoni au wa Peponi?

Jawabu/ Sema: Haijuzu kumuhukukumu mtu kuwa ni wa Peponi au wa Motoni ispokuwa wale ambao dalili zimewaelezea kuwa ni watu wa Peponi, lakini kila mwenye kufanya wema inatarajiwa atapata thawabu na kwayule anaefanya maovu kupata adhabu na tunasema kwamba kila alie kufa akiwa na imani mafikio yake ni Peponi na kila mwwnye kufa katika ushirikina na ukafiri basi atakuwa katika watu wa Motoni, ubaya ulioje wa mafikio hayo.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Muislam anahukumiwa kuwa kafiri kwa sababu ya maasi yake?

Jawabu/ Sema: Hapana Muislam hahukumiwi kuwa kafiri kwa sababu ya maasi anayo yafanya hatakama ni madhambi makubwa midhali sio madhambi ambayo yanamfanya awe kafiri ambayo yameelezwa na sheria katika Qur'an na sunnahh na maswahaba hawakuelezea au maimamuwakubwa, Muislam anabaki kuwa Muumini na anakuwa ni katika wanao muasi Allah katika waislam walio tamka Shahada, mithali hajaingia katika madhambi

yanayo muingiza katika ukafiri au shirki kubwa au unafiki mkubwa.

## Swali/ Ukiulizwa: Je, Maneno yalio tamkwa na ulimi kwa makosa bila kukusudia, au Maneno Machafu yana adhari juu ya tawhiid? Je! mwenye kuyasema hayo yanaweza kumuondoa kunako njia ya Uislam, au ni madhambi madogo?

Jawabu/ Jambo la kutamka na ulimi ni jambo hatari sana kwa tamko moja tu mtu anaingia katika Uislam na mtu anaweza kutoka katika uislam kwa tamko moja tu na Allah atukinge na matamshi ya ulimi ambayo mtu anatamka bila kutarajia yana tofautiana miongoni mwake kuna maneno ya kikafiri ambayo yanayo batilisha Uislam na kuharibu ibada za mtu, kama vile kumtukana Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake, au maneno ya kuwasifu watu wenye cheo na mawalii sifa za Mwenyezi Mungu na kuwaomba msaadana kunasibisha kwao mambo yote ya heri ambayo yanayopatikana kwa wanadamu na katika hayo ni kuwasifu sifa zilizo pindukia zinazo wanyanyua juu ya viumbe wengine na kuwaapia na kufanya masihara sheria ya Mwenyezi Mungu na hukumu zake, au kuchukia hukumu zaMwenyezi Mungu alizo shusha kwa

waja wake, au kupinga hukumu zake alizo zipanga katika matukio yenye kuumiza katika mambo yasiyo pendeza katika mambo yanayo patikana katika dunia kama misiba katika mwili na mali na watoto na mengineyo

Miongoni mwa madhambi makubwa ambayo yanaharibu imani ya mtu na kuiharibu ni kusengenya na Kuteta tunatakiwa tuyatahadhari ukweli wa kutahadhari, tuhifadhi ndimi zetu kutokana na kila tamko ambalo linalo pingana na sheria ya Allah na sunnahh za Mtume wakerehma na amani ziwe juu yake, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Hakika mja anaweza kutamka neno moja linalo mridhisha Allah bila kulichukulia manani, ila Mwenyezi Mungu anamyanyua daraja kubwa na hakika mja anaweza kutamka neno katika maneno yanayo mchukiza Mwenyezi Mungu bila kulichukulia manani anamzamisha kwa sababu ya neno hilo katika Moto wa Jahanam). Imepokelewa na Imamu Bukhari.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Niwakati gani Matendo ya mja yanakatika?

Sema: Haikatiki ibada ya mja ila ni kwa kifo, dalili ni kauli ya Allah mtukifu: { Muabudu Mola wako mpaka kikufikie kifo} (Al-Hijr 99). na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake kutoka kwa Athumani bin Madh'uni wakati alipo kufa: (Ama

Othman Bin Madh'uninamuapa Allah amefikiwa na Umauti). Imetolewa na Imamu Bukhari, na kwakuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuacha kufanya ibada katika maisha yake na maana ya yakini katika aya na hadithi hazina maana ya kufikia daraja ya juu katika Imani ambayo akifikia anaacha kufanya ibada kama wanavyo fasiri baadhi ya watu wanao potosha Dini ya Allah bali yakini inamaana ya kifo.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Nani anae pangilia mambo ya Mbinguni na Ardhini na vilivyomo baina yake?

Jawabu/ Sema: Anaepangilia mambo ya mbinguni na ardhini na vilivyomo baina yake ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika hakuna mfalme asiekuwa Yeye wala hana mshirika wala msaidizi wala anae fanana nae utakasifu ni wake na ametukuka, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na yeye hakuwa na mamlaka yeyote juu yao, ila kwa sababu ya kuwajaribu tujue nani mwenye kuamini akhera na nani anaye tilia shaka. Na Mola wako Mlezi ni mwenye kuhifadhi kila kitu}. (Sabaa 22).

## Swali/ Utakapo ulizwa: ipi hukumu ya mwenye kuitakidi kwamba ulimwengu unpangiliwa na kushiliwa na fito nne au saba , au kwamba kuna vigingi

**vilivyo shikilia kinyume cha Allah, au vinashirikiana na Mwenyezi Mungu?**

Jawabu/ Sema: Mwenye kuitakidi hivyo wanachuoni wamekubaliana kuwa ni kafiri, kwasababu ameitakidi kuwepo mwenyekushiriana na Mwenyezi Mungu katika Uungu wake.

## Swali/ Utakapo ulizwa je, mawalii wanajua ghaibu na kuhuisha wafu?

Jawabu/ Sema: Hakuna anaejua ghaibu ila ni Mwenyezi Mungu na hakuna anae fufua wafu ila ni Mwenyezi Mungu na ushahidi ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ninge jizidishia mema mengi, wala ovu lisinge nigusa. Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mbashiri kwa watu wanao amini} (Aaraf 188) akiwa Mtume rehma na amani zowe juu yake mbora wa viumbe hajuwi ghaibu nani asiekuwa yeye anae stahiki kujua elimu ya ghaibu.

Maimamu wanne ya kwamba yeyote mwenye kutegemea kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake anajua ghaibu au anahuyisha mtu alie kufa, basi huyo atakuwa ametoka katika Uislamu, kwa kumkadhibisha Mwenyezi Mungu ambae alie muamrisha mtume wake aseme kuwambia wanadamu na majini: {Sema: Mimi sikwambiini kuwa ninazo hazina za Mwenyezi Mungu. Wala sijui mambo yaliyo fichikana. Wala sikwambiini

kuwa mimi ni Malaika. Mimi sifuati ila yanayo funuliwa kwangu.} (Al-Anaam 50) na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Hakika kuijua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye ndiye anaye iteremsha mvua. Na anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi. Na haijui nafsi yeyote itachuma nini kesho. Wala nafsi yeyote haijui itafia nchi gani. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujua, Mwenye habari}. (Luqman 34), basi Mtume rehma na amani ziwe juu yake hajui katika elimu ya ghaibu ila yale ambayo aliyo funuliwa Mwenyezi Mungu kwake na akamfundisha na Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuwahi kujidai katika uhai wake hata siku mojakuwa alimuhuyisha yeyote katika maswahaba zake au yeyote katika watoto wake ambao walio kufa kabla yake, hayo yote Mtume hakuyaweza vipi kwa asiekuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

## Swali/ utakapo ulizwa: je, Uwalii ni maalumu kwa watu flani katika baadhi ya Waumini?

Jawabu/ Sema: Kila Muislamu Muumini mchamungu basi mtu huyo kwa Allah ni walii, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika (62) Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu} (Yunus 62-63) Uwalii sio maalumu kwa baadhi ya waislam,

ispokua daraja za uwalii unatofautiana na Maana ya uchamungu: Ni kufanya yale aliyo amrisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake na kujiepusha na yale aliyo yakataza Mwenyezi Mungu na Mtumewake rehma na amani ziwe juu yake na kila muumini uwalii wake ni kwakulingana na kiasi cha uchamungu wake na utekelezaji wake wa ibada.

## swali/ utakapo ulizwa hivi kauli ya Mwenyezi Mungu inayo sema: {Fahamu hakika mawalii wa Mwenyezi Mungu hawana hofu wala hawata huzunika} aya hii inamaana kwamba inajuzu kuwaomba wakiwa hai au wamekufa?

Jawabu/ Sema: Aya hii haina maana ya kuwaomba au kuomba nusra kwao au kuwaomba msaada bali kuna ubainifu juu ya daraja lao na cheo chao na kwamba wao hawatakuwa na hofu duniani na akhera na hawata huzunika katika akhera na katika aya hii kuna kuna wito wakujipamba na tabia za uwalii kwa kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumtii Allah na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake ili kupata habari njema ya kauli ya Mwenyezi Mungu: {Hawatakuwa na hofu wala hawata huzunika} ama kuviomba visivyokuwa Mwenyezi Mungu kufanya hivyo ni ushirikina kama tulivyo bainisha.

## Swali/ Utakapo Ulizwa: hivi wasiokuwa mitume katika mawalii wamehifadhika na kufanya madhambi makubwa na madogo?

Jawabu/ Sema: atakae kuwa walii katika watu wasiokuwa mitume hakika watu hao hawaja takasika na kufanya madhambi makubwa au madogo, hakika wamewahi kuingia katika madhambi wengi katika mawalii wakubwa wa Mwenyezi Mungu wakakosea na kutenda dhambi lakini walifanya haraka kutubia dhambi zao na kuomba msamaha na wakasamehewa na Mwenyezi Mungu.

## Swali/ Je, Hidhri yupo hai mpaka leo?

Jawabu/ Sema: Sahihi ni kwamba hidhri ni Mtume katika mitume wa Mwenyezi Mungu alikufa kabla ya kuzaliwa Mtume muhammad rehma na amami ziwe juu yake, kwasababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: {Nasi hatukumjaalia mwanaadamu yeyote kabla yako kuwa na maishaya milele. Basi je! Ukifa wewe, wao wataishi milele?} (Anbiyaa 34). Laiti angekuwa hai angemfuata Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake na angepigana jihadi na yeye kwasababu Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake ametumwa kwa watu wote na majini wote, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote} (Al-Aarafi 158). Na Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yale alisema: (Hakika nimeonyeshwa katika usiku wenu huu kwamba hakuna kichwa) Imepokelewa na Imamu Bukhari, na hii ni dalili tosha kuwa Hidhri alisha kufa katika wafu na kwakuwa alisha kufa hasikii wito wa yeyote atakae mwita wala hawezi kumuongoa alie potea kunako njia ya haki pindi atakapo muomba amuongoze na visa vinavyo tajwa kuhusu kukutana na baadhi ya watu na visa vya kuonekana kwake na kukaa na baadhi ya watu, hakika visa hivyo ni ndoto na uwongo ulio wazi haumpotezi yule alie pewa na Mwenyezi Mungu elimu akili na busara.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je, walio kufa wanasikia au kujibu kwa mwenye kuwaomba?

Jawabu/ Sema: Walio kufa hawasikii kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: {Hukuwa wewe nimwenye kuwafanya wasikie walioko makaburini} (Faatwir 22) na amesema Mwenyezi Mungi mtukifu: {Kwa hakika wewe huwezi kuwafanya maiti wasikie}. (Namli 80) na maiti hawawezi kumjibu kwa mwenye kuwaomba, Amesema Mwenyezi Mungu: {Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende (13) Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni. Na siku ya kiyama watakataa

ushirikina wenu. Na hapana atakayekupa habari vilivyo kama Yeye Mwenye habari} ( Fatwir 13-14) na kauli ya Mwenyezi Mungu: {Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanao waomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama na wala hawatambui maombi yao} (Ahkaf 5).

## Swali/ Utakapo ulizwa: nikipi ambacho kinacho sikika makaburini kwa baadhi ya walio kufa ambao wanatukuzwa na baadhi ya wajinga?

Jawabu/ Sema: Ni sauti za mashetani wa kijini wanao wapumbaza wajinga ili wajuwe kwamba ni sauti ya maiti alie ombwa ili wawafitinishe na wawapoteze kutokana na dini yao na watu wa makaburini hawasikii wala hawamjibu mwenye kuwaomba au anae waomba kwa ushahidi wa Qur'an Tukufu, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Kwa hakika wewe huwezi kuwafanya maiti wasikie} (Namli 80) na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Mkiwaomba hawasikii maombi yenu} (Fatwir 14) na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Hukuwa wewe nimwenye kuwafanya wasikie walioko makaburini} (Fatwir 22), sasa hao maiti watawajibu vipi ili hali wao wako katika ulimwengu wa Barzakhi, hawana mafungamano yeyote na watu wa duniani amesema Mwenyezi Mungu {Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao

wanao waomba, badala yaMwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama na wala hawatambui maombi yao} (Ahqaaf 5).

## Swali/ ukiulizwa: je maiti katika Mawalii na wengineo wanawajibu walio hai kwa aliyeomba nusra na msaada kwao?

Jawabu/ sema: wao hawajibu mwenye kuwaita na hawawezi kujibu mwenye kuwaomba au akawaomba nusra, amesema Mwenyezi Mungu: {Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende (13) Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni. Na Siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu} (Fatwir 13-14). Hasara ilioje kwa mtu alie danganywa na mashetani na walinganizi wanao potosha waliwapambia ibada za kuwaomba maiti na watu walio zikwa, wakiwemo manabii mawalii na watu wema, amesema Mwenyezi Mungu:{Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanao waomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama na wala hawatambui maombi yao} (Ahqaaf 5).

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi maana ya (Ahyaa) katika kauli ya Mwenyezi Mungu: {Wala kabisa usiwadhanie walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi

**Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi} (Al-Imran 196)?**

Jawabu/ sema: hakika maana ya neno Ahyaa katika aya hiyo nikwamba watakuwa hai uhai wa neema katika kaburi na sio kama maisha ya duniani, kwasababu roho za mashahidi zinaneemeka peponi, kwa sababu hiyo amesema Mwenyezi Mungu: {Kwa Mola wao wanaruzukiwa}. wao katika nyumba ya akhera wana maisha na hali sio kama maisha yao na hali zao duniani. wao hawasikii dua za wenye kuwamba na hawawajibu kama ilivyo tangulia katika aya, hakuna mapishano katika aya, ndio maana katika aya ikaeleza kuwa wanaruzukiwa na siokwamba wao wanatoa rizki.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ipi hukumu ya kukichinjia kisichokuwa Mwenyezi Mungu kwa lengo la kujikurubisha kwa kilicho chinjiwa?

Jawabu/ Sema: hukumu yake ni shirki kubwa, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Swali kwa ajili ya mola wako na uchinje} (Kawthar 2) na kauli ya Mwenyezi Mungu: {Sema: Hakika Sala yangu na ibada zangu na uhai wangu na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote(162) Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyo amrishwa na mimi ni wa kwanza wa

Waislamu} (Al-Anaam 162-163) na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenyezi Mungu amemlaani mwenye kukichinjia kisichokuwa Mwenyezi Mungu) Imepokelewa na Imamu Muslim.

Na kuna kanuni inasema: (kile ambacho kinafanyika kwa ajili ya Allah hiyo ni ibada, kukifanyia kisichokuwa Allah ni ushirikina)

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi Hukumu ya kukiwekea nadhiri kisichokuwa Mwenyezi Munguu Mtukufu?

Jawabu/ Sema: kufanya hivyo ni shiriki kubwa kwa kauli Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenye kuweka nadhiri ya kumtii Mwenyezi Mungu basi amtii na mwenye kuweka nadhri ya kumuasi Mwenyezi Mungu basi asimuasi) Imepokelewa na imamu Bukhari, nadhiri niibada ya kusema na ya kutoa mali au ya kutoa mali au ya kimwili, kulingana na kile alicho kiweka nadhiri na maana ya nadhiri: ni kujilazimisha kufanya jambo ambalo sio lazima kwake kisheria, kwa kutarajia kupata anacho kitarajia au kukinga ambacho ambacho hapendi kimpate, au kwa kushukuru neema iliyo mshukia au janga lililo muondokea nadhiri ni katika ibada ambazo hazijuzu kumfanyia yeyote kinyume cha Mwenyezi Mungu kwasababu Mwenzi mungu amewasifu wenye kutekeleza

nadhiri, akasema Mwenyezi Mungu: {Wanatimiza ahadi,na wanaiogopa siku ambayo shari yake inaenea sana} (Insan 7).

Na kuna kanuni inasema: kila kitendo ambacho amesifiwa na Mwenyezi Mungu mwenye kukitenda basi kimo katika ibada, kile ambacho ni ibada kumfanyia asiekuwa Mwenyezi Mungu ni Ushirikina.

## Sawali/ Utakapo ulizwa: Je, inajuzu kuomba hifadhi kwa asiekuwa Mwenyezi Mungu?

Jawabu/ Sema: linakuwa wazi jawabu kwa kujua aina tatu za kuomba msaada nazo:

1- Kuomba hifadhi kwa kumpwekesha Mwenyezi Mungu kwa kufanya ibada: nako ni kumuomba hifadhi Mwenyezi Mungu kutokana na kila unacho kiogopa. amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa mapambazuko, (1) Na shari ya alivyo viumba, (2)} (Falaqi 1-2) na anasema Mwenyezi Mungu:Sema: Ninajikinga kwa Mola Mlezi wa wanaadamu, (1) Mfalme wa wanaadamu (2) Mungu wa wanaadamu (3) Na shari ya wasiwasi wa Shetani, Khannas}. (Al Nnasi 1-4)

2 - Ni kuomba hifadhi kwa njia ya halali: nako nikuomba hifadhi kwa viumbe walio hai waliopo na

wenye uwezo kukusaidia jambo ulilo waomba na katika yale mambo ambayo yanawezekana kisheria, anasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Mwenyekupata makimbilioau hifadhi basi na akimbilie huko) Imepokelewa na Imamu Muslim.

3 -Kuomba hifadhi kwa njia ya ushirikina: nako ni kukiomba hifadhi kisichokuwa Mwenyezi Mungu katika mambo ambayo hakuna anae yaweza ila ni Mwenyezi Mungu, amesema Mwenyezi Mungu: {Na hakika walikuwako wanaume katika watu walio kuwa wakitafuta kujikinga kwa wanaume wa kijini; kwa hivyo wakawazidisha madhambi} Jinni 6

## Swali/ Utakapo ulizwa: unasema nini unapo fika katika sehemu yeyote?

Jawabu/ Sema: Ninasema yale aliyo niongoza Mtume wa Allah rehma na amani za Allah ziwe juu yake, alisema: (Mwenye kufika katika nyumba yeyote akasema: Ninajikinga kwa maneno ya Mwenyezi Mungu yalio timia kutokana na shari alizo ziumba, hakuna kitakacho mdhuru mpaka atakapo toka katika nyumba hiyo) Imepokelewa na Muslim

## Swali/ utakapo ulizwa: je, inajuzu kuomba nusra kinyume na Mwenyezi Mungu katika yale ambayo hakuna

**anaeyaweza ila ni Mwenyezi Mungu katika mambo yanayo leta heri au kuzuia shari?**

Jawabu/ Sema: kufanya hivyo nikatika ushirikina mkubwa unao tengua matendo ya mwanadamu na unao mtuoa mtu katika dini na kumfanya aishi milele katika moto kwa yule atakae ufanya na hakutubia kabla ya kufa, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba na akaiondoa dhiki} (Namli 62) Maana yake ni kwamba hakuna mwenye uwezo wa kumjibu ila ni Mwenyezi Mungu na hakuna mwenye kuondosha madhara ila ni Mwenyezi Mungu. akawakamea Mwenyezi Mungu kila mwenye kuomba nusrakwa asie kuwa yeye kwa kuanza maneno yake kwa kuuliza, kwa sababu kuomba nusra ni kufanya ibada vilevile kuomba msaada, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Kumbukeni wakati mkiomba nusra kwa Mola wenu mlezi} (Anfal 9) na imethibiti katika sahihi bukhari kutoka kwa Abuu Hurayrah radhi za Allah ziwe juu yake kwamba hakika Mtume rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alisema: nisimkute mmoja wenu atakae kuja siku ya Kiyama akiwa na ngamia anaetoa sauti ya juu, kisha akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu niokoe na ninusuru, ispokuwa nitasema: tayari nimesha kufikishia hakika mimi similiki chochote

katika hilo unalo niomba, nisimkute mmoja wenu anakuja siku ya qiyama akiwa na farasi anaetoa sauti ya chini, kisha anasema: ewe mtume niokowe, nitasema similiki chochote kwa Mwenyezi Mungu nimesha kufikishia, Imepokelewa na Bukhari na Muslim. na ijulikane wazi kuwa inajuzu kuomba nusra kwa wanadamu walio hai ambao tunawaona, sio wale ambao hawapo ikiwa ni katika mambo anayo na uwezo nayo na kuomba nusra kwa mwanadamu allie hai ina maana ya kumuomba msaada, katika yale anayo yaweza kiumbe, kama alivyo omba rafiki wa mussa kwa mussa amsaidie kutokana na adui yao, amesema Allah Mtukufu: {Yule mwenzake alimtaka msaada kumpiga adui yake} (Qaswaswi15) ama kuomba nusra kwa wasiokuwepo miongoni mwa watu na majini na watu wa makaburini wanachuoni wamekubaliana kuwa niharam na nibatili na nikatika Ushirikina.

## Swali/ utakapo ulizwa: je inajuzu kumuabudia kwa majina ya asiekuwa Mwenyezi Mungu kama vile mja wa Nabii au mja wa Hussain na mfano wake?

Jawabu/ sema: Haijuzu kwani wanachuoni wamekubaliana juu ya uharamu wa kila jina linalo abudiwa kinyume cha Mwenyezi Mungu na ni wajibu kubadilisha jina linalo abudiwa kinyume cha

Mwenyezi Mungu, kama jina: Mja wa Nabii, mja wa Mtume, mja wa Hussein na mja wa Al Kaaba na majina mengine mfano wa majina hayo na majina bora na yanayo pendeza kwa Mwenyezi Mungu ni: (Abdullah na Abdurahmani) kama ilivyo kuja katika hadithi sahihi kutoka kwa Mtume rehma na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: (Hakika majina yanayo pendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu ni Abdullah na Abdurahmani) Imepokelewa na Imamu Muslim. ni wajubu kubadilisha majina yanayo abudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu na hii ni kwa wale waliopewa majina hayo na wapo hai walio itwa majina yanayo abudiwa kinyume cha Mwenyezi Mungu.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi hukumu ya kuvaa bangili, au uzi mkononi au shingoni au kumvisha Mnyama au gari au sehemu nyingine kwa ajili ya kuzuia kijicho au husda, au kuondoa mabalaa na shari?

Jawabu/ sema: kufanya hivyo ni ushirikina kwa dalili ya maneno ya Mtume -rehma na amani ziwe juu yake-: (mwenye kuvaa hirizi atakuwa amemshirikisha Mwenyezi Mungu) Imepokelewa

na Imamu Ahmad katika kitabu chake na amesema Mtume -rehma na amani ziwe juu yake-( Isibakishwe katika shingo la ngamia kamba itokanayo na mshale au hirizi lolote ila imekatwa) Imepokelewa na imamu bukhari. na kauli ya Mtume -rehma na amani ziwe juu yake-: (Mwenye kusuka ndevu zake au akavaa kamba ya upinde shingoni au akastanji kwachoo cha mnyama au mfupa hakika Muhammad yuko mbali nae) Imepokelewa na Abuu Daudi, na amesema Mtume -rehma na amani ziwe juu yake-:(Mwenye kuvaa hirizi Mwenyezi Mungu asimtimizie mambo yake) Imepokelewa na Ibn Hibaani katika sahihi yake. Ameenda patupumwenye kutegemea vitu vya upuuzi na uzushi, imekuja katika hadithi: (Mwenye kukitegemea kitu au kukivaa basi ataaegemezewa kwa kitu hicho kimsaidie).

Tiwala: Ni uchawi unaofanywa wakiitakidi kuwa inamfanya mume ampende mke wake, au unawatenganisha na wanafanya uchawi huo kwa lengo la kuleta chuki baina ya wapendanao na watu wakaribu.

Hirizi: ni kitu kinacho vishwa watoto kwa kuzuia kijicho na hasadi

Na maana ya Mahirizi, amesema Almundhiry: (Mahirizi walikuwa wanayavaa wakiona kuwa yanaepusha maafa mbali mbali) na huu ni ujinga na

ni upotevu, kwa sababu sio sababu wala sio sheria kufanya hivyo wala sio Qadar na kuvaa hirizi kunakusanya kuvaa bangilina kuninginiza vitambaa kwa lengo la kuzuia mabalaa na kuleta manufaa kwa mtu, myama gari na nyumba.

## Swali/ Ukiulizwa nini maana ya kutaka Baraka?

Jawabu/ sema: ni kuomba baraka na heri kupitia sababu ambazo anazo zifanya mwanadamu kwa kutarajia kupata heri na makusudio yake na kupata yale anayo yapenda

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je! kutabaruku (kutaka baraka) kupo aina moja au kupo aina nyingi?

Jawabu/ Sema: Kutaka baraka kumegawanyika mara mbili:

1- Kutaka baraka ambako kuna swihi kisheria ambako kumeruhusiwa na Qur'an na Sunnahh juu ya kuswihi kwake na kunufaika mwenye kufanya hivyo na haiswihi kuitakidi kuwepo baraka katika jambo ila iwe ni kwa dalili zilizo thibiti katika Qur'an na Sunnahh, akili haina nafasi katika hilo wala kuliona jambo kuwa linapendeza kufanya hivyo, hatujui kuwa jambo hili kuna baraka ndani yake ila kwa maelezo kutoka kwa muumbaji mwenye hekima mwenye baraka na alie tukuka, au kwa

maelezo kutoka kwa Mtume -rehma na amani ziwe juu yake- kutokana na vitu ambavyo vimetokana na yeye kama vile, nywele na mavazi yake na haya ni maalumu kwa Mtume -rehma na amani ziwe juu yake- na yale yalio thibiti kuwa ameambatana nayo kama nywele na mavazi na watu wazushi wanasema uongo na wanadai kuwa wana nywele za Mtume na nguo zake na haya yote wanayafanya kwa ajili ya kuzichezea akili za baadhi ya waislam na kuharibu dini yao nakuchukuwa dunia yao.

2- Sehemu ya pili: kutaka baraka kuliko katazwa na ilio haramu, ni ile inayo mfikisha mtu katika kumshirikisha Mwenyezi Mungu kama vile kutaka baraka kwa watu wema na vile vinavyo tokana nawao na kutaka baraka kwa makaburi yao kwa kuswali katika makaburiau kuwaomba wakiwa makaburini na kutaka baraka kwa michanga yao kwa kuitakidi kuwa mchanga huo ni dawa na mfano wake ni kutaka baraka na kufanya twawafu au kuvaa vitambaa kwa kila sehemu na mawe na miti akiitakidi kuwa vina ubora na imejulikana kuwa haipatikani chochote kinacho eleza kuwa nisheria kukibusu na kukigusa ila ni jiwe leusi lililopo katika alkaaba na nguzo zake na visivyokua hivyo nimakosa kufanya hivyo kuvigusa na kubusu na kufanya twawafu na kufanya hivyo ni shirki kubwa kwa mwenye kuitakidikuwa vinaleta baraka

vyenyewe, au ni katika shirki ndogo kwa mwenye kudai kuwa ni sababu ya baraka.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Kufuata athari za watu wema na kutabaruku kwa dhati zao na athari zao ni jambo ambalo lipo kisheria au ni uzushi na upotovu?

Jwabu/ Sema: Hii ni itikadi na ibada iliyo zushiwa kwa sababu Maswahaba wa Mtume wetu Muhammad -rehma na amani ziwe juu yake- walikuwa ni wajuzi zaidi na niwatu bora, na niwenye ufahamu zaidi na wanabidii kubwa katika kufanya kheri na niwajuzi wa mambo bora kwa watu wa ubora, hawakutabaruku kwa athari za Abubakari, Omar, Othman na Ally -radhi za Allah ziwe juu yao- na hawakufatilia athari zao ili kutafuta baraka kwao ilihali wao ni watu bora katika Umma huu baada ya manabii, kwa sababu wao walijua kuwa kufanya hivyo ni makosa, na Omar -radhi za Allah ziwe juu yake- alikata mti uliofanyiwa mapatano yalio ridhiwa (Baiatu ridhwan) kwa kuchelea watu wasichupe mipaka kwenye mti huo, na watu wema walio tangulia wao ndio wenye pupa zaidi ya kufanya kheri na laiti ingekuwa kufuata athari za watu wema walio tangulia ni bora basi wangetutangulia kufanya hivyo.

## Swali/ Utakapo ulizwa: inajuzu kutabaruku kwenye Miti au Mawe au Michanga?

Jawabu/ Jawabu: Kufanya hivyo nikatika Ushirikina, imepokelewa kutoka kwa Imamu Ahmad na Tirmidhiy kutoka kwa Abi Waaqid Allaythiy alisema: Tulitoka pamoja na Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwenda khunayni na sisi tukiwa ni waislam wapya na washirikina walikuwa na Mti wa Mkunazi wakiketi chini yake kwa ajili ya kuomba na kutundika silaha zao, Mti huo unaitwa dhatu anwat (Mti wanao tundika juu yake Silaha zao) mara tukapita kwenye Mti wa Mkunazi mwingine tukamwambia Mtume -rehma na amani ziwe juu yake- akawajibu Mtume -rehma na amani ziwe juu yake-: (Allah ni Mkubwa hakika hilo mlilo sema ni mwenendo wa watu wajinga walio pita, nina muapa Allah ambae nafsi yangu iko mikononi mwake, hayo mliyosema ni sawa na yale waliyo sema wana wa Izrael kumwambia Mussa: {Tuwekee waungu tuwaabudu kama makafiri walivyo na miungu, Musa akasema hakika nyinyi ni watu wajinga} (A'araf 138) mtazidi kufuata myenendo ya watu waliokuwa kabla yenu).

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi Hukumu ya kukiapia kisichokua Mwenyezi Munguu Mtukufu?

Jawabu/ Sema: Haijuzu kukiapia kisichokua Mwenyezi Mungu Mtukufu, Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Atakae kuwa ni mwenye kuapa basi aapie kwa jina la Mwenyezi Mungu) Imepokelewa na Bukhari. Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikataza kuapia kisichokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama ilivyo kuja katika kauli ya mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Msiapie kwa majina ya wazazi wenu wala kwa majina ya Matwaghuti) Imepokelewa na Muslim na Matwaghuti: - ni kila kinacho abudiwa kinyume cha Allah, kikiwa kimeridhia au kiongozi asie fuata sheria za Allah au sheria zozote zisizokuwa za Allah- bali mtume rehma na amni ziwe juu yake alijalia kufanya hivyo ni katika shirki, kama ilivyo katika kauli yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenye kukiapia kisichokuwa Mwenyezi Mungu atakuwa amekufuru au amemshirikisha Mwenyezi Mungu) na amesema Mwenyezi Mungu: (Mwenyekuapia kwa uaminifu wake atakuwa sio katika sisi) Imepokelewa na Imamu Ahmad na Ibn Hibani ma Hakim kwa upokezi sahihi.

Muislam ajitahadhari na kuapia kwa jina la Mtume au walii, au kuapia kwa cheo amana na Alkaaba,na mengineyo katika viumbe vya Mwenyezi Mungu.

**Swali/ utakapo ulizwa: Je inajuzu kuitakidi kuwa nyota au sayari zingine zina athari juu ya ulimwengu na watu katika kuleta manufaa na tawfiiki na mafanikio, au kuzuia shari na mambo yanayo chukizwa na Mabalaa.**

Jawabu/ Sema: Haijuzu kuitakidi hivyo kwasababu hivyo havina athari yeyote hata na hakuna wanao sadikisha hayo ila ni watu wenye akili dhaifu, wanaofuata mambo ya kipuuzi na kuitakidi hivyo ni katika ushirikina kwa kauli ya mtume rehma na amni ziwe juu yake katika hadithi Alqudsiyu: (Hakika Mwenyezi Mungu anasema: mwenye kusema mvua imenyesha kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na rehma zake, basi mtu huyo ni mwenye kuniamini na ni mwenye kukufuru uwezo wa nyota na sayari na mwenye kusema Mvua imenyesha kwa sababu ya watu fulani na kwasababu fulani basi huyo atakuwa amenikufuru na anaamini kuwa nyota na sayari zingine zina uwezo wa kudhuru na kunufaisha) Imepokelewa na Bukhari na Muslim na watu wa enzi za ujinga walikuwa wanaitakidi kuwa nyota zina athari katika kunyesha Mvua.

**Swali/ utakapo ulizwa: Je, inajuzu kuitakidi kuwa Abraji (Mistari inayo bainisha njia za jua na nyota na mwezi na sayari zingine) kamavile njia za sayari Dallow na zinginezo kuwa zina athari juu ya yale yanayo mtokea mtu katika maisha yake ikiwemo mafanikio au maovu na inawezekana kujua mambo ya ghaibu yasiyo julikana yatakayo tokea badae kupitia hizo Abraji?**

Jawabu/ Sema: Haijuzu kuitakidi kuwa Abraji (Mistari inayo bainisha njia za jua na nyota na mwezi na sayari zingine) kuwa vina athari ya yanayo mtokea bianadamu katika maisha yake na huwezi kujua yatakayo tokea badae kupitia hizo Abraji kwasababu Elimu yaghaibu ni maalumu kwa Mwenyezi Mungu peke yeke, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Sema ewe Mtume kuwambia watu wako kuwa hakuna anae jua yaliyomo mbinguni wala aridhini katika mambo yasio julikana ila ni Mwenyezi Mungu} (Namli 65) na kwa sababu Mwenyezi Mungu peke yake ndie anae leta manufaa na heri na ndie anae zuia madhara na shari na mwenye kuitakidi kuwa viumbe hivyo vina athari katika kujuwa mambo ya ghaibu na kuleta mafanikio, au mabaya kwa mwenye kuzaliwa katika muda wa kupatikana njia ya sayari hiyo au muda

wa kuonekana kwa sayari Fulani, au akaamini kuwa nyota ina athari katika kuleta manufaa na mafanikio au kuzuia madhara au kumfanya mtu awe muovu, hakika mtu huyo atakuwa amevijalia vitu hivyo kuwa vinashirikiana na Mwenyezi Mungu katika yale ambayo ni haki kwa Mwenyezi Mungu na ni maalumu kwa uungu wake na mwenye kufanya hivyo atakuwa amekufuru, Mwenyezi Mungu atukinge.

## Swali/ utakapo ulizwa: Je ni wajibu kwetu sisi kuhukumiana kwa yale alio teremsha Mwenyezi Mungu Mtukufu?

Jawabu/ Sema: Ni wajibu kwa waislam wote kuhukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, kwa kauli yake Mwenyezi Mungu: {Na wahukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao. Nawe tahadhari nao wasije kukufitini ukaacha baadhi ya aliyo kuteremshia Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka, basi jua kwamba hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao. Na hakika wengi wa watu ni wapotofu } (Maida 49) na Mwenyezi Mungu amewatia aibu wote wenye kufuata sheria zilizotungwa na viumbe kwa kusema kwake: {Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini? } (Maida 50).

## Swali/ Utakapo ulizwa ni ipi maana ya shafaa (Uombezi)?

Jawabu/ sema: Shafaa ni kumtumia mtu akuombee kwa lengo la kupata manufaa na kheri, au kuzuia madhara na shari

### Swali/ Utakapo ulizwa: Ni aina ngapi za Shafaa?

Jawabu/ Sema: Shafaa (Uombezi) una aina tatu:

1- Uombezi ulio thibitishwa ambao hauombwi kwa yoyote ila ni kwa Mwenyezi Mungu, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Sema ewe Mtume hakika Mwenyezi Mungu ndio mwenye idhini ya uombezi wote} (Zumar 44) nao ni uombezi maalumu kwa ajili ya kusalimika na adhabu ya moto na kufuzu kupata neema za peponi na uombezi huo una masharti mawili:

A- Idhini kwa muombaji ili aweze kuomba, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake} (Albaqara 255).

B- Ni kuridhiwa kwa yule anae ombewa, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {na hawataomba ila kwa yule alie ridhiwa} (Anbiyaa 28) na amekusanya Mwenyezi Mungu masharti yote katika kauli yake: {Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipo kuwa baada ya Mwenyezi Mungu kutoa idhini

kwa amtakaye na kumridhia} (Najmu 26) atakae taka apate uombezi basi amuombe Mwenyezi Mungu Mtukufu, yeye ndie mmiliki wa uombezi huo na ndie mwenye idhini nao na asiombe uombezi kwa mtu mwingine kwa kauli ya mtume –rehma na amani ziwe juu yake-: (Utakapo omba muombe Mwenyezi Mungu) Imepokelewa na Tirmidhiy, basi mja anatakiwa aseme pindi akiomba: Ewe Mwenyezi Mungu nijalie katika wale watakao kuwa katika uombezi wa Mtume wako rehma na amani ziwe juu yake siku ya Qiyama.

2- Uombezi ulio kataliwa nao ni ambao una tafutwa kwa asiekuwa Mwenyezi Mungu katika mamabo ambayo hakuna mwenye uwezo nayo ila ni Mwenyezi Mungu nao ni uombezi wa kishirikina.

3- Uombezi wa kidunia baina ya waja nao ni Uombezi baina ya viumbe walio hai katika dunia katika yale mambo ambayo wanayoyaweza na wanayahitaji baadhi yao kwa wengine katika mahitaji ya kidunia na uombezi huu unapendekezwa pindi utakapo kuwa ni katika mambo ya heri na ni haramu ikiwa itakuwa katika shari, kama ilivyo katika kauli ya Mwenyezi Mungu: {Mwenye kusaidia msaada mwema ana fungu lake katika hayo na mwenye kusaidia msaada muovu naye ana sehemu yake katika hayo} (Nisaa 85).

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je, shafaa huombwa kwa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake na Manabii na watu wema na mashahidi kwasababu wao watawafanyia watu shafaa siku ya Qiyama?

Jawabu/ Sema: Uombezi ni milki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: {Sema hakika Mwenyezi Mungu ndio mmliki wa uombezi wote} (Zumar 44) uombezi tunamuomba Mwenyezi Mungu kwani ndie mmiliki na ndie anae toa idhini kwa kumtii Mtume wake –rehma na amani ziwe juu yake- ambae alie sema: (Utakapo omba muombe Mwenyezi Mungu) Imepokelewa na Tirmidhiy, Basi tunatakiwa kusema: Ewe Mwenyezi Mungu tujalie katika wale watakao kuwa katika uombezi wa Mtume wako rehma na amani ziwe juu yake siku ya Qiyama.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi hukumu ya mwenye kuwafanya wafu kuwa waombezi baina yao na Allah Mtukufu katika kuhakikisha wanapata maombi yake?

Jawabu/ Sema: Hii ni katika ushirikina mkubwa, kwasababu Mwenyezi Mungu Mtukufu amekemea mwenye kujalia baina yake na Mwenyezi Mungu uombezi mwingine, amesema Mwenyezi Mungu

Mtukufu: {Nao, badala ya Mwenyezi Mungu, wanaabudu wasio wadhuru wala kuwanufaisha na wanasema: Hawa ndio waombezi wetu kwa Mwenyezi Mungu! Sema: Je! Mnamwambia Mwenyezi Mungu asiyo yajua ya katika mbingu wala katika ardhi? Subhanahu wa Taa'la! Ametakasika na ametukuka na hao wanao mshirikisha naye} (Yunus 18) na akawaita Mwenyezi Mungu kuwa ni washirikina kwa kusema: {kwa vile wanavyo mshirikisha} na akawahukumu kuwa nimakafiri pindi alipo sema: {Hakika Mwenyezi Mungu hamuongoi alie muongo na kafiri} (Zumar 3) na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu akiwaelezea maneno yao kuhusu waombezi wao: {Na wale wanao wafanya wenginewe kuwa ni walinzi wakisema: Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu} (Zumar 3).

**Swali/ Utakapo ulizwa: Je, inafahamika kutokana na kauli ya Allah Mtukufu: { Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangelikujia, wakamuomba Mwenyezi Mungu msamaha na Mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangelimkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu} (An Nisaa: 64). Inamaana**

**ya kuomba msamaha kwa Mtume -rehma na amani ziwe juu yake- mpaka baada ya kufa?**

Jawabu/ Sema: Hakika kuomba waombewe msamaha na Mtume rehma na amani ziwe juu yake- ni maalumu katika wakati wa uhai wake Mtume -rehma na amani ziwe juu yake- na sio baada ya yeye kufa na haikuthibiti kutoka kwa maswahaba au karne bora habari yeyotesahihi kwamba wao walikuwa wakimuomba Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- awaombee msamaha baada ya kufa kwake na kwasababu Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- wakati Bi Aisha –radhi za Allah ziwe juu yake- alipo muomba Mtume amuombee dua na amuombee msamaha baada ya kufa kwake, Mtume alimwambia: (Hilo nitalifanya nikiwa hai nitakuombea msahamaha na kukuombea). Imepokelewa na Bukhari, hadithi hii inatafsiri Aya, hakika kumuomba Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- akuombee msamaha inakuwa katika wakatiwa uhai wake, na sio baada ya kifo chake na haikuripotiwa kumuomba Mtume amuombee msamaha yeyote baada ya kifo chake, ispokuwa kwa watu walio kuja baada ya kumalizika karne bora ya Maswahaba na Mataabiina na ilikuwa kwa sababu ya kuenea ujinga na uzushi katika dini, baadhi ya watu wakafanya hivyo wakipingana na muongzo wa maswahaba na watu

wema walio tangulia walio na elimu na maimamu wa uongofu katika Maswahaba na walio kuja baada ya Maswahaba na walio wafuata kwa wema.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Enyi watu } (Maida 35)?

Jawabu/ Sema: Maana yake ni kujikurubisha kwake kwa kumtii na kumfuata Mtume –rehma na amani ziwe juu yake-, hii ndio njia ambayo ameiamrisha Mwenyezi Mungu ili tujikurubishe kwake, kwa sababu maana ya Wasila: ni kitu kinacho kufikisha katika mambo unayoyahitaji na huwezi kuyafikia unayo yahitaji ispokuwa ni kwa kufanya aliyo yaamrisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake, ikiwemo kumpwekesha na kufanya ibada na sio kufuata njia inayo kufikisha kuwaomba wanadamu wenzako kama mawalii na walio zikwa makaburini, kufanya hivyo ni kugeuza maana halisi ya wasila na kuviita vitu majina ambayo sio majina yake na kwa.hakika kufanya hivyo hivyo ni udanganyifu kutoka kwa Mashetani wa kibinadamu na wakijini kwa lengo la kuwapoteza watu kunako njia ya uongofu inayo mfikishamtu peponi.

## Swali/ Ukiulizwa nini maana ya Tawassulu?

Jawabu/ Sema: Asili katika Twasulu ni kujikurubisha na katika sheria: Ni kujikurubisha kwa Mwenyezi

Mungu Mtukufu kwa kumtii na kumuabudu na kumfuata Mtume wake –rehma na amani ziwe juu yake- na kufanya kila anayo yapenda Mwenyezi Mungu na kuyaridhia.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni aina ngapi za Tawassuli?

Jawabu/ Sema: Tawasulu ina aina mbili: Iliyo ruhusiwa kisheria na Iliyo katazwa.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi Tawassuli iliyo ruhusiwa?

Jawabu/ Sema: (A) ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kutumia majina yake, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Mwenyezi Mungu ana majina mazuri muombeeni kupitia majina hayo} na sifa zake, kama ilivyo kuja katika kauli ya Mtume – rehma na amani ziwe juu yake-: (Ewe ulie hai na mwenye kusimamia mambo yote ninaomba nusra kwa rehma zako). Huku ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kupitia sifa yake ya rehma.

(B): Kutawasul kwa Mwenyezi Mungu kwa kutumia matendo mema yaliofanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ambayo inaafikiana na mafundisho ya Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- kama anae sema: Ewe Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi yangu kwako na kwa kufuata sunnah zaMtume wako –rehma na amani ziwe juu yake- niponye na

uniruzuku na kama kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake –rehma na amani ziwe juu yake-, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumemsikia mwenye kuita akiitia Imani kwamba: Muaminini Mola wenu Mlezi; nasi tukaamini. Basi tusamehe madhambi yetu na utufutie makosa yetu na utufishe pamoja na watu wema.} (Al-Imrani 193) na baada ya tawasuli hii walimuomba Mwenyezi Mungu kwa kusema: {Mola wetu Mlezi! Na utupe uliyo tuahidi kwa Mitumewako, wala usituhizi Siku ya Kiyama. Hakika Wewe huvunji miadi.} (Al Imrani194) kama walivyo jikurubisha kwa Mwenyezi Mungu watu wa pangoni walio funikwa na jiwe kupitia matendo yao mema ili Mwenyezi Mungu awaondoshee matatizo yao, kama ilivyo kuja katika hadithi ya Ibn Omar –radhi za Allah ziwe juu yake- ambayo ipo katika sahihi Bukharin a Muslim kwamba Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- aliwaelezea watu kuhusu kisa cha watu watatu ambao walio zibwa na jiwe kubwa wakiwa pangoni, wakamuomba Mwenyezi Mungu kupitia matendo yao mema awaondoshee matatizo.

(C): Kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kupitia dua za mja mwema, ambae yupo hai na anaweza kuomba dua hiyo, kama anavyo omba mtu kwa mwenzake amuombee dua na kama maswahaba walivyo muomba Abasi awaombee kwa Allah ili

ateremshe mvua na Omar Bin Khatwabi alimuomba Uweisi Alqarniy amuombee dua, na kama ilivyo kuja kwa watoto wa Yaaqubu walimuomba baba yao awaombee msamaha, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Ewe babaetu tuombee msamaha hakika sisi tulikosea} (Yusuf 97)

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi Tawassulu ilio katazwa?

+Jawabu/ sema: ni tawasulu ambayo sheria imebatilisha, kama anae jikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kupitia walio kufa na kuwaomba msaada na uombezi na huko ni kutawasulu kishirikina kwa makubaliano ya wanachuoni wa ummah huu, hatakama wanao ombwa ni manabiiau mawalii, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na wale wanao wafanya wengine kuwa ni walinzi wakisema: Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu} (Zumar 3) kisha akafatisha kutoa sifa zao na hukumu yao kwa kusema: {Hakika MwenyeziMungu atahukumu baina yao katika wanayo khitalifiana. Hakika Mwenyezi Mungu hamwongoi aliye mwongo kafiri} (Zumar 3) akawahukumu kuwa ni makafiri na kuwa wametoka katika dini,na vile vile katika tawasulu iliyo katazwa ni ile ambayo imenyamanziwa na sheria, kwababu tawasulu ni ibada na ibada huwezi

kuifanya mpaka ifundishwe, miongoni mwa tawasulu hizo zilizo katazwa ni kamavile kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa cheo cha Mtume kwa watu maalumu, au vitu vingine mfano wake na kama kauli za baadhi ya watu: Ewe Allah nisamehe kwa cheo cha Mtume, au ewe Allah nakuomba kupitia Mtume wako au cheo cha watu wema au kwa mchanga wa mtu flani, hakika haya hayakuwekwa na Mwenyezi Mungu na mtume wake na kwasababu hiyo yanakuwa uzushi na ni wajibu kujiepusha nayo na haikupokelewa kutoka kwa watu wema walio tangulia miongoni mwa maswahaba na mataabii na maimamu viongozi Radhi za Allah ziwe juu yao.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni aina gani ya kuzuru makaburi kwa wanaume?

Jawabu/ sema: Kuzuru Makaburi kumegawanyika katika sehemu mbili:

1- Ziara ya Makaburi ya kisheria ambayo anapata malipo mwenye kuifanya. Ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:

(A) inakukumbusha akhera, kwa kauli ya Mtume – rehma na amani ziwe juu yake-: (Nilikuwa nimemukatazeni kuzuru makaburi basi yatembeleeni kwasababu yanawakumbusha akhera) Imepokelewa na Muslim.

(B) Kuwasalimia walio kufa na kuwaombea dua, unasema: (Amani ziwe juu yenu watu wa nyumba za waumini...nk.) kwa salam hiyo ananufaika mwenye kutembelea makuburi na alie tembelewa.

2- Ziara ambazo hazikuelezwa kisheria mwenye kufanya hivyo anapata dhambi nayo ni ziara inayo kusudiwa ndani yake kuwaomba waliopo makaburini, au kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwao na huu ni uzushi mkubwa ambao unampelekea kuingia katika ushirikina au kuomba nusra kwa waliokufa na kuwaomba uombezi na msaada na hii ndio shirki kubwa kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: {Huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Ufalme ni wake. Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ngozi ya kokwa ya tende (14) Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni. Na Siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu. Na hapana atakaye kupa habari vilivyo kama Yeye Mwenye habari} (Fatwir 13-14).

## Swali/ Utakapo ulizwa: unasema nini unapokuwa umezuru makaburi?

Jawabu/ Sema: Ninasema yale aliyo waelekeza Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- Maswahaba zake pindi wanapo tembelea makaburi waseme: (Amani ziwe juu yenu watu wa nyumba za waumini mmepata yale mliyo ahidiwa

kesho mapema na Mwenyezi Mungu akipenda tutawafuata) Imepokelewa na Imamu Muslim, kisha nawaombea kwa Mwenyezi Mungu rehma na msamaha na daraja ya juu na mambo mengine katika dua nzuri.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Tunajikurubisha kwa Allah kwa kuomba dua kwenye makaburi ya watu wema?

Jawabu/ sema: ikiwa atamuomba Mwenyezi Mungu akiwa katika makaburi ya watu wema atakuwa amefanya uzushi na ni njia ya kumpelekea afanye ushirikina na imepokelewa kutoka kwa Ally Bin Hussain –radhi za Allah ziwe juu yake- kuwa alimuona mtu anamuomba Mwenyezi Mungu kwenye kaburi la Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- akamkataza na akasema: hakika Mtume –radhi za Allah ziwe juu yake- alisema: (Msilifanye kaburi langu kuwa sikukuu) Imetolewa na dwiyaa Almaqdisiy katika kitabu(Almukhtaar 428).na kaburi tukufulillilo beba mwili mtukufu na twahara na mwanadamu bora kwa Mwenyezi Mungu ni kaburi la Mtume muhammad –radhi za Allah ziwe juu yake-na hakuna upokezi wowote sahihi ulio julikana kutoka kwa yeyote katika maswahaba –radhi za Allah ziwe juu yao- kwamba alikuwa akiliendea kaburi la Mtume –radhi za Allah ziwe juu yake-kisha akamuomba Mwenyezi Mungu akiwa

kwenye kaburi hilo, vile vile mataabii na walio fuata maswahaba kwa wema, hawakuwa wanaenda kumuomba Allah kwenye makaburi ya maswahaba na watu wakubwa katika ummah huu, kwa hakika kufanya hivyo ni ushawishi wa shetani ambao ulio wavaa baadhi ya watu wasio na maarifa katika nyakati zilizo tangulia, wakaliona jambo hilo kuwa ni zuri ilihali watu wema walio tangulia waliliona ni baya na wakajiepusha na jambo hilo na kulikemea vikali, kwa kutambua ubaya wake na mwisho wake, baadhi ya watu walio pita wakaghafilika kwa sababu ya elimu zao ndogo akili ufahamu na darja zao, wakaangukia katika kamba za Shetani zikawapelekea kuona uzushi ni jambo jema na kutumbukia katika Ushirikina, Allah atukinge.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi maana ya Al-Ghuluwwu na je! ipo aina tofauti?

Jawabu/ Sema: Ghuluwwu: ni kuvuka mipaka ya kisheria kwa kuvuka yale aliyo yaamrisha Mwenyezi Mungu na inakuwa kwa kuzidisha juu ya ibada uliyo amrishwa kufanya kisheria au kupewa idhini na pia inakuwa kwa kuacha kwa njia ya kufanya ibada.

Na katika aina ya kuvuka mipaka kwenye kuangamiza: ni kuvuka mipaka kwa Manabii na watu wema kwa kuwanyanyua daraja zaidi ya wanavyo stahiki na kuwapenda kupindukia zaidi ya

wanavyo stahili na kuwapa sifa ya Uungu, au kuwafanyia chochote katika ibada na kuwapa sifa nyingi ambazo zinawafanya wawe katika daraja ya Uungu.

Na katika kuvuka mipaka: kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa kuacha moja kwa moja mambo ya halali ambavyo ameviumba Mwenyezi Mungu kwa masilahi ya watu, ikiwemo vyakula na vinywaji na vile anavyo hitaji mwanadamu katika usingizi na kuoa au kuolewa.

Na katika kuvuka mipaka kunako chukiza zaidi: ni kuwahukumu Waislamu wenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu kuwa ni makafiri na yanayo fanana na hayo ikiwemo kuwatenga na kuwahama na kuwapiga vita, kuwafanyia uadui na kuhalalisha heshima, mali na damu zao.

## Swali/ Utakapo ulizwa: taja chochote katika dalili za kisheria zinazo tahadharisha kuvuka mipaka?

Jawabu/ Sema: dalili zimekuwa nyingi katika kitabu na Sunnah ambazo zinazo kataza mtu kuvuka mipaka na zina tahadharisha jambo hilo, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na mimi sio miongoni mwa wenye kujikalifisha} (Swad 86) na Mwenyezi Mungu amewakataza wana wa Izraeli kuhusu kuvuka mipaka katika dini, alisema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Msivuke mipaka

katika dini yenu} (Nisaa 171) na amesema Mtume –rehma na amani ziwe juu yake-: (Tahadharini na kuvuka mipaka hakika kuliwaangamiza waliokuwa kabla yenu) Imetolewa na Ahmad na amesema Mtume –rehma na amani ziwe juu yake-: (Wameangamia wenye kuvuka mipaka, wameangamia wenye kuvuka mipaka, wameangamia wenye kuvuka mipaka) Imepokelewa na Muslim.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je, inajuzu kufanya twawafu sehemu ambayo siyo katika Al Kaabah?

Jawabu/ Sema: haijuzu kufanya twawafu katika sehemu isiokuwa Alkaaba, kwa sababu Mwenyezi Mungu mshindi mwenye nguvu amehusisha kufanya twawafu iwe kwa ajili ya Al Kaaba, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na ili wafanye twawafu kwenye nyumba tukufu} (Hajji 29) na Mola wetu hakuturuhusu kinyume na hayo, kwasababu twawafu ni ibada na Mwenyezi Mungu ametutahadharisha kuzua ibada yeyote, haturuhusiwi kufanya ibada ila kwa dalili sahihi katika kitabu naSunnah, kuzua ibada bila dalili ya kisheria nikufanya uaduina Mwenyezi Mungu na ibada kumfanyia asiekuwa Mwenyezi Mungu ni ushirikina unao haribu ibada zote na kunamtoa mtu katika dini takatifu na kumfanya awe kafiri, Mwenyezi Mungu atukinge.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Inajuzu kusafiri sana (mara kwa mara) kwenda kuadhimisha eneo na sehemu ambayo siyo Misikiti mitatu (Msikiti Mtukufu wa Makkah na Msikiti wa Mtume Madina na Masjidul Aqswaa)?

Jawabu/ Sema: haijuzu kusafiri kwa ajili ya kuadhimisha eneo na sehemu kwa kuitakidi kuwa ni bora kusafiri kwenda huko ispokuwa Misikiti mitatu, kwa kauli ya Mtume -rehma na amani ziwe juu yake-: haifungwi safari ila kwa kutembelea Misikiti mitatu: Msikiti mtukufu wa Makkah na Msikiti wangu huu (Msikiti Mtukufu wa Madina) na Msikiti wa Aqswaa) (unapatikana palestina) Imepokelewa na Imamu Muslim.

**Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Hadithi hizi zifuatazo ni sahihi au ni za uongo anazuliwa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake?: (Mambo yatakapo kuwieni mazito basi ni juu yenu kuzuru makaburi) na (Mwenye kuhiji kisha asinizuru hakika amenihama (yuko mbali nami) na (Mwenye kunizuru na akamzuru Baba yangu Ibrahim ndani ya mwaka mmoja nimemdhaminia Pepo kwa Allah) na (Mwenye kunizuru baada ya kufa kwangu ni kama aliyenizuru katika uhai wangu) na (Mwenye kuitakidi katika jambo basi limemnufaisha) na (Fanyeni Tawassuli kwa (utukufu) jaha yangu kwasababu jaha yangu mbele ya Allah ni kubwa) na (Mja wangu amenitii basi ninakufanya ni miongoni mwa wanaosema kukiambia kitu kuwa na kikawa) na (Hakika Mwenyezi Mungu ameumba viumbe kutokana na nuru ya Mtume wake Muhammad**

**rehma na amani za Allah ziwe juu yake).**

Jawabu/ Sema: Hadithi zote ni hadithi za kumzulia na kumsemea uongo Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- na hadithi hizi zinaenezwa na watu wa bidaa na wanao abudu makaburi na ambae anapotaka kitu husema kuwa na kinakuwa ni Mwenyezi Mungu ni mwenyezi Muungu peke yake hana mshirika na hana mfano wa kitu chochote, utakasifu ni wake na sifa kamilifu ni zake, hazistahiki wala hamiliki yeyote si manabii wala mawalii, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Hakika amri yake anapo taka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa} (Yasin 82) {Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote} (A'araaf 54) Ametanguliza yale ambayo yangecheleweshwa kutajwa ili ifidishe mjumuiko na mjumuiko huo ni wa viumbe vyote na mipango yote ni ya Mmwenyezi Mungu peke yake hana mshirika.

**Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Inajuzu kuzika maiti Misikitini na kujenga Misikiti kwenye makaburi?**

Jawabu/ Sema:hiyo ni katika mambo mazito ya haramu na ni uzushi wenye hatari kubwa na ni katika njia kubwa zinazo mpelekea kuingia katika ushirikina, kutoka kwa Mama Aisha –radhi za Allah

ziwe juu yake- alisema: alisema Mtume –rehma na amani ziwe juu yake-katika maradhi ya kifo chake maradhi ambayo hakupona: (Mwenyezi Mungu amewalaani mayahudi na manaswara walio yafanya makaburi ya manabii zao kuwa ni Misikiti) alisema Aisha –Radhi za Allah ziwe juu yake-: (Yatahadharishwe yale walio yafanya) Imepokelewana Bukharin a Muslim, kutoka kwa Jundubi Bin Abdillah –radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- alisema kabla ya kukata roho kwa siku tano: (Fahamuni hakika walio kuwa kabla yenu walikuwa wanayafanya makaburi ya manabii wao na watu wema ni misikiti, fahamuni msiyafanye makaburi kuwa misikiti, hakika mimi nawakataza hilo), Imepokelewa na Muslim. Na misikiti iliyo jengwa juu ya makaburi haiswihi wala haijuzu kuswali ndani yake na pindi msikiti utakapo jengwa juu ya kaburi au makaburi ni wajibu kubomoa msikiti, ama ukijengwa Msikiti juu ya sehemu isiyokuwa makaburi kisha akazikwa maiti ndani yake msikiti haubomolewi, lakini ni wajibu kaburi kufunguliwa na kuhamishwa alie zikwa ndani yake kutoka msikitini kwenda katika makaburi ya watu wote.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi Hukumu ya kuyajengea makaburi?

Jawabu/ Sema: kujengea makaburi ni uzushi (Bid'a) yenye kuchukiza kwa yaliyomo kutokana na kuvuka

mipaka katika kuwatukuza walio zikwa katika hayo makaburi na jambo hilo linapelekea kufanya ushirikina, ni wajibu kuondoa yote yaliyo jengwa juu ya makaburina kufanywa sawasawa kwa kumaliza na kutokomeza Bid'aa zote bila kuzipa sababu zote ambazo zinazo pelekea kufanya ushirikina, amepokea Imamu Muslim katika sahihi yake kutoka kwa abii Hayaji Al-Asadiy Hayaan Bin Huswayni alisema: aliniambia Ally –radhi zaAllah ziwe juu yake-: je! Nisikutume kwa yale aliyo nituma Mtume –rehma na amani ziwe juu yake-: (Usiache picha yeyote ila umeifuta wala kaburi lililo inuliwa ila umeisawazisha).

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Mtume rehma na amani ziwe juu yake alizikwa Msikitini?

Jawabu/ sema: Alizikwa katika chumba cha Aisha –radhi za Alla ziwe juu yake- na kaburi lake limekuwa nje ya msikiti kwa zaidi ya miaka (80) na akaupanua Msikiti wa Mtume mmoja katika viongozi wa Umawiyyah kikawa kile chumba cha Aisha kana kwamba kiko katika Msikiti na Yule kiongozi hakukubali makatazo na makemeo na matahadharisho ya kuingizwa chumba katika msikiti yalio tolewa na wanachuoni wa zama zake na amesema Mtume–rehma na amani ziwe juu yake- akiwa ni mwenye kutahadharisha kujengwa misikiti juu yamakaburi: (Fahamuni hakika walio

kuwa kabla yenu walikuwa wanayafanya makaburi ya manabii wao na watu wema ni misikiti, fahamuni msiyafanye makaburi kuwa misikiti, hakika mimi nawakataza hilo) Imepokelewa na Imamu Muslim na Mtume –rehma na amani ziwe juuyake- aliwalaani wenye kuyafanya makaburi kuwa misikiti kama ilivyo kuja katika hadithi ambayo imepokelewa na watu wa sunani. Na yametokea yale aliyo yachelea Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- juu ya umati wake na yametokea yale aliyo yatahadharisha kwasababu ya kuzidiwa na ujinga na kudanganywa na mashekhe wa kizushi na Bid'a, wakawa wanajikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kufanya yale ambayo ni yakumfanyia uadui Mwenyezi Mungu na yanapingana na muongozo wa Mtume wake –rehma na amani ziwe juu yake- ikiwemo kuweka makaburi misikitini na kuyajengea na kuyawekea stara juu yake na kuyatandikia na kuyafanyia twafu (Kuzunguka makaburi kwa lengo la ibada) na kuweka masanduku ya kuyatolea nadhiri, zikaenea shirki mbalimbali na mambo ya upotevu kwajina la kuwapenda watu wema na kuwaheshimu na kutaka hao walio zikwa wawaelekeze kwa Mola wa walimwengu wote ili waweze kujibiwa matakwa yao na yote hayo ni katika mirathi ya upotevu wa watu walio tangulia, amesema Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- (Mtafuata myenendoya waliokuwa kabla yenu

hatua kwa hatua mpaka wangiliingia ndani shimo la mburu kenge mtaingia) Imepokelewa na Bukhari na Muslim.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake yupo hai kaburini mwake na kwamba hutoka kwa watu katika maulidi kwa kile kinacho semwa kuwa anahudhuria kama wanavyo itakidi baadhi yao?

Jawabu/ Sema: wamekubaliani Maimamu wane na Ummah kwa ujumla juu ya kuwa maswahaba -radhi za Allah ziwe juu yao- hawakumzika Mtume – rehma na amani ziwe juu yake- mpaka roho yake ilipo achana na kiwiliwili chake, kwasababu haingii akilini kumzika akiwa hai!! Na kwamba wao walimchagua kiongozi wa Mtume baada yake na mwanae Fatma –radhi za Allah ziwe juu yake- aliomba mirathi yake kwa mtume na haikunukuliwa kwa yeyote katika maswahaba na matabii na walio kuja baada ya mataabii katika maimamu wanne kwamba Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- alitoka kaburini mwake baada ya kufa Maswahaba wakamzika tena, atakae dai kwamba Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- anatoka kaburini na kuwaendea watu mtu huyo atakuwa mzushi na muongo, kachezewa na mashetani na atakuwa ni mwenye kumzulia

Mwenyezi Mungu na juu ya Mtume wake –rehma na amani ziwe juu yake- itawezekana wapi ilihali Mwenyezi Mungu anasema: {Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwisha pita kabla yake Mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma?} (Al-Imrani144) na anasema pia: {Kwa hakika wewe utakufa na wao watakufa} (Zumar30), Mwenyezi Mungu akakutanisha habari ya kifo cha Mtume wake –rehma na amani ziwe juu yake- na kifo cha watu wote ili ibainike kwamba nikifo cha kweli na ambacho mtu anahama kutoka katika nyumba ya dunia kwenda katika nyumba ya barzakhi (Kaburini) ambapo hakuna kutoka mpaka siku ya qiyama kwa ajili ya hesabu, malipo baada ya kufufuliwa na kutoka makaburini na miongoni mwa majibu ambayo yanayo nasibiana na hao wajinga na wapotoshaji ambao wanaitakidi kufufuka kwa Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- ni maneno aliyoyasema Imamu Qurtubiy almaliky aliefariki mwaka (656)H katika kitabu chake (Almufhim an khur'afati khurujih swalAllah alayhi wasalam min Qabrihi) Maana ya kitabu hiki:-majibu yenye kufahamisha kuhusu uzushi wa kutoka kwa Mtume kaburini mwake- alisema: (Kusema kuwa Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- anafufuka katika kaburi lake inaonyesha kuwa amesha haribika kwa akili ya kawaida na inalazimika juu ya Mtume –rehmana amani ziwe juu yake- akitoka kaburini basi

kaburi lake libaki tupu kutokana na mwili wake na kusibaki chochote katika kaburi lake, baada ya hapo litembelewe kaburi likiwa halina kitu, ni lisalimiwe ilihali halina kitu, kwa sababu akisha toka Mtume kaburini inajuzu kumuona usiku na mchana na muda wote awe katika hali ya kawaida kama viumbe wengine na anaesema kuwa Mtume anafufuka hayo ni mambo ya kijinga hata mwenye akili ndogo hawezi kuyaamini na kushikamana nayo). Mwisho wa kunukuu.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni nini Bidaa? Na ni zipi aina zake? Na ni ipi hukumu ya kila moja? Na je! Katika Uislamu kuna bidaa nzuri?

Jawabu/ Sema: Bid'aa ni ibada ambayo mwanadamu amemuabudu mola wake bila dalili ya kisheria inayo muongoza kufanya ibada hiyo nayo imegawanyika katika sehemu mbili:

1- Bida'a inayo mkufurisha mtu, mfano wa kutufu kwenye makaburi kwa kujikurubisha kwa alielazwa kaburini.

2- Bida'a ambayo anapata dhambi mwenye kuifanya bila ya kukufuru, mfano wa kufanya maulidi ya Mtume au ya Walii bila maulidi hiyo kuwa na mambo kishirikina na mambo ya kikafiri na katika Uislam hakuna bida'a nzuri, kwa sababu kila bida'a niupotovu, kwa ushahidi wa kauli ya Mtume

– rehma na amani ziwe juu yake-: (tahadharini na mambo ya uzushi, kwasababu kila mambo ya uzushi ni Bida'a na kila bida'a ni upotevu) na katika upokezi mwingine: (Kila upotevu unampelekea mtu kuingia motoni) Imepokelewa na Imamu Ahmad na Annasaiy na Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- hakutoa katika Bida'a chochote na bida'a zote ni haramu na mwenye kufanya bida'a (Uzushi katika dini) halipwi thawabu, kwasababu nikukosowa ibada zilizo wekwa kisheria na nikuzidishakatika dini, baada ya ukamilifu na kutimia wake na mambo yote ya Bida'a hurudishwa kwa aliye yafanya, kwa ushahidi wa kauli ya Mtume –rehma na amani ziwe juu yake-: (Mwenye kufanya ibada yeyote ambayo haipo katika dini yetu basi atarudishiwa mwenyewe) Imepokelewa na Imamu Muslim. Na kauli ya Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- (Mwenye kuzua katika dini yetu yale ambayo hayamo katika dini basi atarejeshewa mwenyewe)Imepokelewa na Bukharin a Muslim na maana ya dini yetu: yaani Uislam.

**Swali/ Utakapo ulizwa: Inafahamikaje kauli ya Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Mwenye kuweka**

**Sunnah iliyokuwa nzuri anamalipo yake na malipo ya mwenye kuifanya Sunnah hiyo)?**

Jawabu/ Sema: (Mwenye kuanzisha Sunnah nzuri) yaani mwenye kufanya ibada ilio letwa na Uislam na ikawa watu wameisahau, au akalingania kufanyia kazi yale yaliokuja katika Qur'an na Sunnah, katika mambo ambayo watu wengi hawayajuwi basi mtu huyo atapata malipo na malipo ya mwenye kumfuata, kwasababu hadithi hii sababu yake ni kulingania watu watoe sadaka ili ziwasaidie masikini ambao waliokuwa wakiomba msaada na aliesema: (Mwenye kuanzisha Sunnah nzuri), ndie alie sema: (Kila Bida'a ni upotevu) na Sunnahhchanzo chake ni Qur'an na sunnahh na Bida'a haina asili katika Qur'an wala katika sunnahh, bali Uzushi ni jambo ambalo akili za baadhi ya watu walio kuja baada ya mtume na maswahaba zimeliona ni zuri lakini halina asili katika Qur'an na Sunnah.

**Swali/ Utakapo ulizwa: Inafahamikaje kauli ya Omar radhi za Allah ziwe juu yake: (Neema ya Bidaa) na kuzuka kwa Adhana ya pili siku ya Ijumaa wakati**

**wa Othman radhi za Allah ziwe juu yake?**

Jawabu/ sema: hakika kauli ya Omar –radhi za Allah ziwe juu yake- (Uzuri ulioje wa Bida'a) inakusudiwa Maana ya bida'a katika lugha ya kiarabu na siyo maana yake katika sheria, kwasababu Omar –radhi za Allah ziwe juu yake- alisema maneno yale akikusudia swala ya tarawehe ambayo iliyo anzishwa na Mtume -rehma na amani ziwe juu yake –ikawa kitendo cha Omar kinakubaliana na kitendo cha Mtume - rehma na amani ziwe juu yake - na kitendo chochote ambacho kina huyisha kitendo cha Mtume - rehma na amani ziwe juuyake – sio Bida'a bali ni kukiendeleza na kuhuyisha na kukumbusha watu wayafanye yale yalio achwa na kusahaulika na nikulingania watu wafanye jambo la kisheria ambalo amelilingania Mtume – rehma na amani ziwe juu yake - na akalifanya, ama kitendo cha Othmani –radhi za Allah ziwe juu yake- hakika yeye ni katika watu ambao Mtume - rehma na amani ziwe juu yake – aliwalingania watu wafuate sunnahh zake pamoja na makhalifa wote walio bakia wakati alipo sema Mtume- rehma na amani ziwe juu yake-: (Ni juu yenu kufuata mwenendo wangu na mwenendo wa makhalifa viongozi) na wasiokuwa makhalifa viongozi hawana daraja hilo kwasababu Mtume- rehma na amani ziwe juu yake -aliwataja makhalifa ndio wafuatwe na hakutaja wengine, walikuwa maswahaba –radhi za Allah

ziwe juu yao- ni wenye kutahadharisha zaidi Bida'a na mambo ya uzushi na miongoni mwao ni Ibn Masuudi – radhi za Allah ziwe juu yake-alisema kuwambia watu walio zua katika dini wakati wanapo mtaja Mwenyezi Mungu kwa pamoja na kwa namna maalumu walio jiwekea ili hali malengo yao wanakusudia heri: (Mumemtangulia Muhammad na Maswahaba zake kielimu, au mmeleta Uzushi na dhulma!) na walipo mwambia: (Tulikusudia heri na thawabu) aliwambia: (Sio kila mwenyekutaka heri anaipatia) imepokelewa na Daramiy katika Sunani yake na kuna maswahaba wengi walikuwa wanapendelea sana kusema pindi wanapo kaa na wenzao: (Fuateni na msizue) na alisema Ibn Omar –radhi za Allah ziwe juu yake-: (Kila Bida'a ni upotevu hatakama watu watauona nzuri).

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume ni Sunnah au ni bidaa?

Sema: Kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume (Maulidi) haikuja katika Kitabu wala katika Sunnah haina dalili ya kisheria na haikuthibiti hata kwa mmoja katika Maswahaba radhi za Allah ziwe juu yao na hajesema kuhusu maulidi yeyote katika Wanachuoni (viongozi) wanne, ingekuwa ni jambo la heri na twaa wangetutangulia kulifanya. Na wanasema watu wa kusherehekea maulidi ya

kwamba wao wanasherehekea kuzaliwa kwa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake kwasababu ya kuonyesha na kudhihirisha mapenzi juu yake, lakini kumpenda Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake ni faradhi ya lazima juu ya kila Muislamu haifai kumuamini isipokuwa kwa kumpenda rehma na amani za Allah ziwe juu yake na yanakuwa mapenzi kwa kumtii na siyo kwa kusherehekea kuzaliwa kwake na wa kwanza kufanya bidaa hii ni Ubeidiyyiina Al Baatwiniyyah mazandiki wanaoitwa Faatwimiyyuuna na hiyo ni baada ya kufa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake kwa karne nne na wanasherehekea watu wa maulidi siku ya jumatatu ambayo ni siku aliyofariki Mtumerehma na amani za Allah ziwe juu yake na ukweli ni kwamba kusherehekea kuzaliwa kwake Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake hakupo isipokuwa ni kuwaiga Manaswara wanavyo sherehekea kuzaliwa kwa Nabii Issa amani ya Allah iwe juu yake, Mwenyezi Munguamekwisha tutosheleza kunako bidaa na uzushi na ubunifu wa umamah potofu kwa kutuletea sheria safi iliyo timia na sifa zote njema anastahiki Allah Mola wa viumbe wote.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi hukumu ya kujifunza uchawi, au kufanya kazi ya uchawi?

Sema: Haijuzu kujifunza uchawi wala kuufanyia kazi na kufanya uchawi ni ukafiri kwa kauli yake Allah Mtukufu: {Na wakafuata yale waliyo zua mashetani kuuzulia ufalme wa Suleiman. Na wala Suleiman hakukufuru, bali mashetani ndio walio kufuru, wakiwafundisha watu uchawi na yaliyo teremshwa kwa Malaika wawili, Haaruta na Maaruta katika Baabil. Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru. Wakajifunza kwa hao wawili yale ya kumfarikisha mtu na mkewe. Wala hawawezi kumdhuru mtu ila kwa kutaka Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza yatayo wadhuru wala hayawanufaishi. Na hakika wanajua kwamba aliye hiari na haya hatakuwa na fungu lolote katika akhera} (Al Baqarah: 102) na kauli yake Allah Mtukufu: {Wanaamini masanamu na Shetani} (Al Nnisaa: 51).

Al Jibti: Wametafasiri wanachuoni kuwa ni uchawi, Allah ameunganisha uchawi na twaghuti (shetani), kama ilivyo kwamba kuamini twaghuti (shetani) ni ukafiri, vilevile kuufanyia kazi uchawi ni ukafiri, ni lazima kumkataa shetani na kuitakidi kwamba uchawi ni batili na kwamba ni elimu chafu yenye kuharibu dini (ya mtu) na dunia pia na ni wajibu kujiepusha na kujiweka mbali nayo na watu wake.

Amesema Allah Mtukufu: {Na shari ya wanao pulizia mafundoni} (Al Falaq: 4) na amesema Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Jiepusheni na mambo saba yenye kuangamiza) akataja miongoni mwa hayo ni uchawi na katika hadithi: (Mwenye kufunga fundo kisha akapuliza ndani yake hakika amefanya uchawi na mwenye kufanya uchawi amefanya ushirikina) ameipokea Al Nnasaai na amepokea Al Bazzaar: (Si katika sisi mwenye kutuhumu au kutuhumiwa mikosi kwa kurusha ndege au kwa mwenye kufanya au kufanyiwa ukuhani, aumwenye kufanya uchawi au kufanyiwa uchawi) na adhabu ya mchawi ni kuuliwa hakika Omar Bunil Khatwab radhi za Allah ziwe juu yake aliwaandikia viongozi ya kwamba (Muuweni kila mchawi mwanaume na mchawi mwanamke) ameipokea Bukhar na kutoka kwa Jundubi radhi za Allah ziwe juu yake amesema Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Hukumu ya mchawi ni kuchinjwa) ameipokea Tirmidhiy, hakika Hafswa radhi za Allah ziwe juu yake alimuuwa mjakazi wake baada ya kumroga (kumfanyia uchawi).

**Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Wanavyofanya watu wa mazingaombwe ya kujichoma (kwa**

**visu) na kula vitu vigumu ni uchawi na mazingaombwe au ni makarama?**

Sema: Wanayofanya watu wa mazingaombwe miongoni mwa yaliyo tajwa ni katika mambo wanayo saidiana na mashetani kivitendo na baadhi yake hufanyiwa uchawi macho ya watu, wakaona yale yasiyo ya kweli kwamba ni ukweli, kama wachawi (wa Firauni) walivyo mfanyiaMussa amani ya Allah iwe juu yake na watu walioshuhudia tukio ambalo Allah amelitaja katika Qur'ani na hakika lilionekana mbele Mussa kama kweli ya kwamba kamba zao za kichawi zinaenda mbio na ukweli ni kwamba haziendi mbio, kama alivyosema Allah Mtukufu: {Akasema: Bali tupeni nyinyi! Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio} (Twaha: 66), lau watu wa mazingaombwe (kiini macho) wakisomewa Ayat Kursiyy na Suratul Falaq na Surat Nnaas na Suratul Faat'ha na mwisho wa Suratul Baqarah na nyenginezo miongoni mwa Aya za kubatilisha uchawi na mazingaombwe (viini macho) kwa idhini ya Allah Mtukufu, vinakuwa wazi viini macho vyao bandia na uongo wao na kudhihiri kwa watu ubatili wao na uongo wao.

Na makarama hayawi isipokuwa kwa watu wema wenye kumpwekesha Allah, walio salimika kutokana na bidaa na uzushi na karama ni heri kumfikia Muumini na kukingwa na shari na wala hii

haimaanishi kwamba yeye ni bora kuliko wengine katika Waumini ambao hawana karama na karama inatakiwa ifichwe iwe siri na sio kutangaza, wala hailiwi watu wakadanyika kwayo.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi hukumu ya kwenda kwa mchawi kwa ajili ya tiba?

Sema: Haijuzu kumwendea mchawi mwanaume au mchawi mwanamke kumuuliza au kutaka tiba kwao, kutokana makatazo ya Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake juu ya hilo na dalili ni baada ya kuulizwa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake kuhusu "Al Nnashrah" ambayo ni kuondoa uchawi kwa kutumia uchawi akasema: (Hayo ni miongoni kazi za shetani) yaani "Al Nnashrah" ameipokea Abuu Daud, wala hakijuzu chochote katika kazi za shetani wala hakupatikani manufaa ndani yake wala hamna heri yeyote.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi namna ya kujikinga kutokana na uchawi kabla haujakupata na ni ipi tiba yake ukikupata?

Sema: Ni kudumu na Adhkari (nyiradi) za asubuhi na jioni na hasa uradi usemao: (Bismi LLahi ladhii laa yadhurru maa ismihi shay un fil ardhwi walaa fiy ssamaa wahuwa Ssamiiul A'liim), mara tatu

asubuhi na jioni na kusema: (Audhu bikalimaati LLahi taammaatmin sharri maa khalaqa) na uwatakie hifadhi ahli (mke) na watoto kwa kusema: (Ui'dhukum bikalimaati LLahi taammah min kulli shaytwaani wa haammah wamin kulli a'ynin laammah) kama ilivyo katika hadithi na kusoma Suratu Ikhlas (Qul huwa LLahu) na (Qul Audhubi Rabbil Falaq) na (Qul Audhubi Rabbil Nnaas) mara tatu asubuhi na jioni na Aayat Kursiyy na Abili za mwisho za Suratul Baqarah usiku na kula tende saba asubuhi.

Na baada ya kupatwa na uchawi: Ni kumsomea aliyerogwa Aya za Qur'ani moja kwa moja na dua zilizothibiti katika sunnah ya Mtume na hijama(kuumika) na kuharibu nyenzo zote alizo fanyiziwa uchawi wakati wa kuziondoa na utabatilika uchawi na kupona aliyerogwakwa idhini ya Allah.

**Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Inajuzu kwenda kwa kuhani na watu wa kutazamia nyota na wenye kusomea vikombe au kiganja na wenye kudai kwamba wana elimu ya mambo yajayo kwa unajimu (kutumia nyota) na**

**kwamba wanajua mambo ya mawinguni?**

Sema: Kuwaendea hao na kuwauliza pamoja na kusikiliza uongo wao ni haramu isipokuwa kwa mwenye kukusudia kudhihirisha uongo wao na kufedhehesha ushenzi wao na kuuweka wazi uchafu wao kwa Wanachuoni wenye kuweza kulifanya hilo na ni wajibu kuhadharisha watu kutokana na kila anaedai kwamba anajua mambo ya ghaibu (yaliyo fichikana) na kutahadharisha na ushenzi wao na udanganyifu wao kwa walioghafilika, ewe uliye pata hasara mwenye kukubali uongo wao na batili yao uzushi wao, amesema Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Mwenye kumwendea mganga wa kienyeji (mshirikina) au kuhani akayaamini yale anayosema basi amekwisha kufuru yale aliyo teremshiwa Muhammad rehma na amani za Allah ziwe juu yake) wameipokea Ahlu Sunana. na amesema Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Mwenye kumuendea mganga (mshirikina) akamuuliza jambo (mtu huyo) hatokubaliwa Swala siku arobaini) ameipokea Muslim.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Unasema nini katika hadithi hii: (Jifunzeni uchawi wala msifanye uchawi)?

Sema: Hadithi hii ni ya uongo na anazuliwa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake, vipi akataze uchawi kisha awambie watu wajifunze huo uchawi.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni watu gani ambao ni bishara bora baada ya Manabii?

Sema: Ni Maswahaba radhi za Allah ziwe juu yao na hiyo ni kwamba ilipokuwa Mtume wetu Muhammad rehma na amani za Allah ziwe juu yake ni mbora wa Manabii wamekua Maswahaba (wake) ni bora kuliko Maswahaba wa Mitume wote na mbora wao ni Abubakar amesema Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Halija chomoza jua wala kuzama baada ya Manabii na Mitume (hajatokea) mtu bora kuliko Abubakar) kisha Omar kisha Othman kisha Ally radhi za Allah ziwe juu yao, kisha Maswahaba kumi (waliobashiriwa Pepo). Na Maswahaba wanapendana, kwa ajili hiyo Ally radhi za Alla ziwe juu yake aliwapa wanae majina ya Makhalifa walokua kabla yake, miongoni mwa majina ya wanae ni Abubakar na Omar na Othman na amekadhibisha mwenye kusema: ya kwamba Maswahaba hawawapendi Waumini miongoni

mwa Ahlali Baiti na kwamba Ahlali Baiti hawawapendi Maswahaba, haya ni katika uzushi wa maadui wa Ahlali Baiti na maadui wa Maswahaba radhi za Allah ziwe juu yao.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni nini wajibu wetu kwa Maswahaba radhi za Allah ziwe juu yao na ni ipi hukumu ya kumtukana mmoja wao?

Sema: Ni wajibu kuwapenda na kuwaheshimu na kuwakirimu wote na kuwaridhia wote, kwa sababu Mwenyezi Mungu amewaridhia na hakumbagua hata mmoja kati yao; kama alivyosema Allah Mtukufu: {Na wale walio tangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari na waliowafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa} (Taubah: 100) na akasema Allah Mtukufu: {Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waumini walio fungamana na wewe chini ya mti} (Al Fat'hi: 18) na akasema Allah akiwazungumzia: {Na wote hao Mwenyezi Mungu amewaahidia wema.} (Al Hadid: 10) na ni wajibu kuwapenda wake wa Mtume (Mama za Waumini) na kuwaheshimu na ni haramu kumtukana mmoja waokwasababu hilo ni katika madhambi makubwa; amesema Allah Mtukufu: {Na wake zake ni mama zao} (Al Ahzaab: 6), basi

wake wa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake wote ni Mama za Waumini kwasababu Allah hakutofautisha hata mmoja kati yao, imekuja katika hadithi ya Abii Said Al Khudriy radhi za Allah ziwe juu yake amesema: Amesema Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Msiwatukane Maswahaba zangu lau mmoja wenu atatoa dhahabu mfano wa mlima wa Uhudi hawezi kufikia kibaba alichotoa Swahaba wala nusu yake) amepokea Bukhari na Muslim.

Wala si ajabu kutokana na nafasi yao hii tukufu, kwani wao wamezitoa nafsi zao na mali zao ili kuinusuru dini ya Allah na wakawapiga vita wale wenye kupinga ulinganizi wa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake walio karibu na walio mbali, wakazihamanchi (zao) katika njia ya Allah na wao ndio sababu ya kila heri inayo patikana katika umma mpaka siku ya Qiyama, wana mfano wa malipo kwa waumini wote watakaokuja baada yao mpaka Allah atakapo irithisha ardhi na walio juu yake, hawakuwepo mfano wao katikaumma uliopita kabla yao wala hawata patikana baada yao, radhi za Allah ziwe juu yao na awaridhie na ole wao wale wenye kuwafanyia uadui na kuwatukana na kuwatia ubaya na kuwatia aibu.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi adhabu ya mwenye kumtukana mmoja kati ya

**Maswahaba wa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake- au akamtukana mmoja kati ya wakeze Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake?**

Jawabu/ Sema: Adhabu yake ni kulaaniwa na kutolewa na kuwekwa mbali na rehma ya Allah, amesema Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Mwenye kuwatukana Maswahaba zangu iwe juu yake laana ya Allah na Malaika na watu wote), ameipokea Twabraany na lililo la wajibu ni kumpinga kwa nguvu zote mwenye kumtukana mmoja kati ya Maswahaba au mwenye kumtukana mmoja kati ya wake wa Mtume radhi za Allah ziwe juu yao wote na ni wajibu kwa kiongozi wa kanda maalum kumtia adabu kisawa sawa na kumuadhibu mwenye kufanya hivo.

## Swali/ Utakapo ulizwa: Je, inajuzu kusema kwamba watu wote ni dini moja?

Jawabu/ Sema: Haijuzu kusema hivi wala kuitakidi hivi na hiyo ni katika aina kubwa za ukafiri nako ni kumkadhibisha Allah na kupinga hukumu yake na kulinganisha katika ya ukafiri na Imani na kulinganisha kati ya haki na batili, na vipi atie shaka mtu mwenye akili juu kubatilisha jambo la kuweka sawa na kuchanganya kati ya Dini ya Allah na dini

potofu ya matwaguti? Na vipi itakuwa pamoja Tauhidi na shirki, haki na batili?basi dini ya Uislamu ndiyo dini ya haki na isiyokuwa hiyo ni batili, hakika Allah amekwisha ikamilisha dini yake na akatimiza neema zake, amesema Allah Mtukufu: {Leo nimekukamiliishieni dini yenu na nimekutimizieni neema yangu na nimekupendeleeni Uislam ndiyo dini ya kweli} (Al Maida: 3), haijuzu kupunguza kitu katika Uislamu wala kuongeza, au kuulinganisha na dini nyingine katika dini za kikafiri na dini za matwaghuti au kuzichanganya pamoja na haifai kwa Muislamu mwenye akili kuitakidi kuwa hii inajuzu wala kujishughulisha (kwenda mbio) katika hilo mtu mwenye chembe ya akili na imani, amesema Allah Mtukufu: {Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye akhera atakuwa katika wenye kukhasiri} (Al Imrani: 85) na amesema Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Naapa kwa yule ambae nafsi ya Muhammad ipo mikononi mwake hatonisikiliza mimi yeyote katika umma huu awe Yahudi au Naswara, kisha akafa bila ya kuamini yale nilitumwa nayo isipokuwa atakuwa ni katika watu wa Motoni) ameipokea Muslim.

## Swali/ Utakapo ulizwa: ni yapi matunda ya kumuamini Allah na kumpwekesha na kusimama (kuwa na msimamo) katika kufuata sunnah za

## Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake?

Jawabu/ Sema: Wenye imani iwe ni mtu mmoja au jamaa wanahakikishiwa kila heri duniani na akhera kwa kufunguliwa baraka kutoka mbinguni na ardhini, anasema Allah Mtukufu: {Na lau kuwa watu wa miji wangeli amini na wakamchamungu, kwa yakini tungeli wafungulia baraka kutoka mbinguni na katika ardhi. Lakini walikanusha basi tukawapatiliza kwa sababu ya yale waliyo kuwa wakiyachuma} (Al A'araf: 96).

Na vilevile kwa imani ya uhakika mtu hupata utulivu wa nafsi na amani ya akili na moyo kukunjuka, anasema Allah Mtukufu: {Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua} (Ra'ad: 28) .Muumini mwenye kumpwekesha Mola wake na mwenye kufuata sunnah za Mtume wake kwa dhati na ukweli huishi maisha mazuri (na atakuwa) ni mwenye akili salama yenye neema mwenye utulivu wa moyo hana dhiki ya nafsi wala huzuni, wala hatenzwi nguvu na shetanikwa kutiwa wasiwasi na hofu na huzuni, wala hakati tamaa wala hapati tabu katika dunia yake na akhera atakuwa na furaha katika Pepo yenye neema, anasema Allah Mtukufu: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke naye akawa ni Muumini,tutamhuisha

maisha memema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda} (An Nahli: 97).

Basi fanya pupa ndugu yangu Muislamu mwanaume na mwanamke ili uwe miongoni mwa watakaofuzu katika bishara hii wenye kuingia katika ahadi hii ya Mola Mtukufu.

# Hitimisho

Ndugu yangu mtukufu ... Dada yangu mtukufu

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye ametukamilishia dini na akatutimizia neema na akatuongoza katika dini ya Uislamu dini ya haki na Tauhidi na furaha ya duniani na akhera.

Na jambo la muhimu- enyi wakarim- ni kwenda mbio katika kuzidisha kutafuta elimu ya kisheria yenye kuegemea katika Kitabu na Sunnah kwa ufahamu za wale walioridhiwa na Allah na wao wapo radhi naye, ili tuwe miongoni mwa wenye kumuabudu Allah kwa elimu natusalimike kutokana na kuingia katika shubuhaati na upotevu na fitina, na kila mmoja vyovyote atakavyo kuwa na cheo cha juu lakini ameamrishwa kuitafuta elimu na ni muhitaji mkubwa wa elimu.

Na huyu ndiye Mtume wako rehma na amani za Allah ziwe juu yake, Mola wake alimuamrisha kusoma; amesema Allah Mtukufu: {Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu} (Muhammad: 19) na akamuongoza kumuomba Mola wake ziada ya elimu; amesema Allah Mtukufu: {Na sema: Mola wangu Mlezi! Nizidishie elimu} (Twaha: 114). Basi jitahidi ewe uliye kuwafikishwa (uliye jaaliwa) kufuata mwongozo wa Mtume wako na Imamu wako Muhammad rehma na amani za Allah ziwe juu yake, na bishara ya heri

na utukufu ni katika nyumba mbili (Peponi), amesema Allah Mtukufu: { Mwenyezi Mungu atawainua walio amini miongoni mwenu na walio pewa elimu daraja za juu. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayo yatenda} (Al Mujadalah: 11).

Na baada ya kusoma, kuwa pamoja na wenye kuifanyia kazi elimu (wenye kuyafanyia kazi waliyo yasoma), na jitahidi kueneza heri na elimu ili ukutane na msafara wa watu wema wenye kutengeneza (palipo haribika), na upate malipo juu ya wale uliowalingania, nauandikiwe thawabu kutokana na yule aliyekuaitikia, na hakuna kilicho bora baada faradhi kuliko jambo la kueneza elimu na kulingania katika heri.

Ni ukubwa ulioje wa athari za walinganizi katika haki juu ya watu, wao ni waokozi kwa idhini ya Allah kwa yule aliye zama katika kiza cha ujinga na upotevu na uzushi, wao ndio wenye kuwashika mikono na kuwaelekeza katika njia ya amani na nuru na uongofu na njia ya Peponi. Na sifa zote njema anastahiki Allah Mola wa viumbe wote.

# Yaliyomo

Utangulizi wa Shekh Swalah Al-Budayri .................. 1
Utangulizi wa watunzi................................................ 3
Swali/ Utakapo ulizwa: Nanai Mola wako?............... 6
Swali/ Utakapo ulizwa ni kwa kitu gani umemjua Mola wako mlezi?........................................................... 6
Swali/ Utakapo ulizwa ni ipi dini yako? .................... 7
Swali/ Utakapo ulizwa ni zipi nguzo za Imani?......... 8
Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kumuamini Mwenezi Mungu Mtukufu?...................................... 9
Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kumuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu Mtukufu?.................. 9
Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kuamini vitabu vilivyo shushwa? .................................................... 10
Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kumuamini Manabii na Mitume? ............................................. 12
Swali/ Utakapo ulizwa: vipi inakuwa kuamini siku ya mwisho?........................................................... 13
Swali/ Utakapo Ulizwa: Je Adhabu za kaburi na neema zake zimethibiti katika Qur'an na sunnah?............... 14
Swali/ utakapo ulizwa: Hivi waumini watamuona mola wao siku ya Qiyama? ............................................ 16
Swali/ Utakapo ulizwa: Kuamini Hukumu ya Mwenyezi Mungu na Qadar zake inakuwa vipi?..... 17
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Mwanadamu anaendeshwa katika mambo yote anayo yafanya au amekhiyarishwa? ........................................................................ 18
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Inaswihi imani bila Matendo?........................................................... 19
Swali/ Utakapo ulizwa ni zipi nguzo za Uislam?..... 19
Swali/ utakapo ulizwa: ni ipi maana ya shahada kuwa hapana Mungu apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mungu mmoja na kwamba Muhammad nimtume wa Mwenyezi Mungu?............................................... 20
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni yapi masharti ya Lailaha ila Allah? ........................................................................ 21
Swali/ Utakapo ulizwa: Nani Mtume wako? ........... 25
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni kipi cha kwanza alicho faradhisha Mwenyezi Mungu kwa waja wake? ....... 26
Swali/ Utakapo ulizwa: Mwenyezi Mungu ameumba viumbe kwa sababu gani? ...................................... 26

Swali/ Ukiulizwa: Nini maana ya Ibada?................ 27
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Dua ni katika Ibada?..... 27
Swali/ utakapo ulizwa: ni yapi masharti ya kukubaliwa ibada kwa Allah Mtukufu?.................................... 29
Swali/ Utakapo Ulizwa: Je, inajuzu kuwa na imani njema bila ya matendo?.......................................... 30
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni zipi aina za Tawhiid?.... 30
Swali/ Utakapo ulizwa ni ipi dhambi kubwa ambayo aliasiwa Mwenyezi Mungu kwayo?........................ 32
Swali/ Utakapo ulizwa ni vingapi vigawanyo vya Ushirikina? ........................................................... 33
Swali/ Utakapo ulizwa: ni zipi aina za Ukafiri?....... 35
Swali/ Utakapo ulizwa: ni zipi aina za Unafiki?...... 36
Swali/ Utakapo ulizwa ni vitu gani vinavyo tengua Uislam?.......................................................... 37
Swali/ Ukiulizwa: inajuzu kumuhukumu mtu duniani kuwa ni mtu wa motoni au wa Peponi?.................. 43
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Muislam anahukumiwa kuwa kafiri kwa sababu ya maasi yake?. ................. 43
Swali/ Ukiulizwa: Je, Maneno yalio tamkwa na ulimi kwa makosa bila kukusudia, au Maneno Machafu yana adhari juu ya tawhiid? Je! mwenye kuyasema hayo yanaweza kumuondoa kunako njia ya Uislam, au ni madhambi madogo? ................................................ 44
Swali/ Utakapo ulizwa: Niwakati gani Matendo ya mja yanakatika?.......................................................... 45
Swali/ Utakapo ulizwa: Nani anae pangilia mambo ya Mbinguni na Ardhini na vilivyomo baina yake?...... 46
Swali/ Utakapo ulizwa: ipi hukumu ya mwenye kuitakidi kwamba ulimwengu unpangiliwa na kushiliwa na fito nne au saba , au kwamba kuna vigingi vilivyo shikilia kinyume cha Allah, au vinashirikiana na Mwenyezi Mungu?............................................ 46
Swali/ Utakapo ulizwa je, mawalii wanajua ghaibu na kuhuisha wafu?...................................................... 47
Swali/ utakapo ulizwa: je, Uwalii ni maalumu kwa watu flani katika baadhi ya Waumini?..................... 48
swali/ utakapo ulizwa hivi kauli ya Mwenyezi Mungu inayo sema: {Fahamu hakika mawalii wa Mwenyezi Mungu hawana hofu wala hawata huzunika} aya hii

inamaana kwamba inajuzu kuwaomba wakiwa hai au wamekufa?........................................................... 49
Swali/ Utakapo Ulizwa: hivi wasiokuwa mitume katika mawalii wamehifadhika na kufanya madhambi makubwa na madogo?............................................ 50
Swali/ Je, Hidhri yupo hai mpaka leo?.................... 50
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, walio kufa wanasikia au kujibu kwa mwenye kuwaomba?............................ 51
Swali/ Utakapo ulizwa: nikipi ambacho kinacho sikika makaburini kwa baadhi ya walio kufa ambao wanatukuzwa na baadhi ya wajinga? ...................... 52
Swali/ ukiulizwa: je maiti katika Mawalii na wengineo wanawajibu walio hai kwa aliyeomba nusra na msaada kwao?.............................................................. 53
Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi maana ya (Ahyaa) katika kauli ya Mwenyezi Mungu: {Wala kabisa usiwadhanie walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi} (Al-Imran 196). .......................................... 53
Swali/ Utakapo ulizwa: ipi hukumu ya kukichinjia kisichokuwa Mwenyezi Mungu kwa lengo la kujikurubisha kwa kilicho chinjiwa?...................... 54
Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi Hukumu ya kukiwekea nadhiri kisichokuwa Mwenyezi Munguu Mtukufu.. 55
Sawali/ Utakapo ulizwa: Je, inajuzu kuomba hifadhi kwa asiekuwa Mwenyezi Mungu? ......................... 56
Swali/ Utakapo ulizwa: unasema nini unapo fika katika sehemu yeyote? .................................................... 57
Swali/ utakapo ulizwa: je, inajuzu kuomba nusra kinyume na Mwenyezi Mungu katika yale ambayo hakuna anaeyaweza ila ni Mwenyezi Mungu katika mambo yanayo leta heri au kuzuia shari? ................ 57
Swali/ utakapo ulizwa: je inajuzu kumuabudia kwa majina ya asiekuwa Mwenyezi Mungu kama vile mja wa Nabii au mja wa Hussain na mfano wake?......... 59
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi hukumu ya kuvaa bangili, au uzi mkononi au shingoni au kumvisha Mnyama au gari au sehemu nyingine kwa ajili ya kuzuia kijicho au husda, au kuondoa mabalaa na shari? ......................................................................... 60
Swali/ Ukiulizwa nini maana ya kutaka baraka? ..... 62

Swali/ Utakapo ulizwa: Je! kutabaruku (kutaka baraka) kupo aina moja au kupo aina nyingi?...................... 62
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, Kufuata athari za watu wema na kutabaruku kwa dhati zao na athari zao ni jambo ambalo lipo kisheria au ni uzushi na upotovu? ....................................................................... 64
Swali/ Utakapo ulizwa: inajuzu kutabaruku kwenye Miti au Mawe au Michanga?.................................. 65
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi Hukumu ya kukiapia kisichokua Mwenyezi Munguu Mtukufu? ............... 66
Swali/ utakapo ulizwa: Je inajuzu kuitakidi kuwa nyota au sayari zingine zina athari juu ya ulimwengu na watu katika kuleta manufaa na tawfiiki na mafanikio, au kuzuia shari na mambo yanayo chukizwa na Mabalaa. ....................................................................... 67
Swali/ utakapo ulizwa: Je, inajuzu kuitakidi kuwa Abraji (Mistari inayo bainisha njia za jua na nyota na mwezi na sayari zingine) kamavile njia za sayari Dallow na zinginezo kuwa zina athari juu ya yale yanayo mtokea mtu katika maisha yake ikiwemo mafanikio au maovu na inawezekana kujua mambo ya ghaibu yasiyo julikana yatakayo tokea badae kupitia hizo Abraji? ........................................................ 68
Swali/ utakapo ulizwa: Je ni wajibu kwetu sisi kuhukumiana kwa yale alio teremsha Mwenyezi Mungu Mtukufu?................................................. 69
Swali/ Utakapo ulizwa ni ipi maana ya shafaa (Uombezi)?......................................................... 70
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, shafaa huombwa kwa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake na Manabii na watu wema na mashahidi kwasababu wao watawafanyia watu shafaa siku ya Qiyama?............ 72
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi hukumu ya mwenye kuwafanya wafu kuwa waombezi baina yao na Allah Mtukufu katika kuhakikisha wanapata maombi yake? ....................................................................... 72
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, inafahamika kutokana na kauli ya Allah Mtukufu: { Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangelikujia, wakamuomba Mwenyezi Mungu msamaha na Mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangelimkuta Mwenyezi

Mungu ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu} (An Nisaa: 64). Inamaana ya kuomba msamaha kwa Mtume -rehma na amani ziwe juu yake- mpaka baada ya kufa? ........................................... 73
Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Enyi watu } (Maida 35)? ......................................................................... 75
Swali/ Ukiulizwa nini maana ya Tawassulu?........... 75
Swali/ Utakapo ulizwa: ni aina ngapi za Tawassuli?76
Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi Tawassuli iliyo ruhusiwa?............................................................. 76
Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi Tawassulu ilio katazwa? ......................................................................... 78
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni aina gani ya kuzuru makaburi kwa wanaume? ....................................... 79
Swali/ Utakapo ulizwa: unasema nini unapokuwa umezuru makaburi? ................................................ 80
Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Tunajikurubisha kwa Allah kwa kuomba dua kwenye makaburi ya watu wema? 81
Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi maana ya Al-Ghuluwwu na je! ipo aina tofauti? ............................................ 82
Swali/ Utakapo ulizwa: taja chochote katika dalili za kisheria zinazo tahadharisha kuvuka mipaka? ......... 83
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, inajuzu kufanya twawafu sehemu ambayo siyo katika Al Kaabah?.................. 84
Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Inajuzu kusafiri sana (mara kwa mara) kwenda kuadhimisha eneo na sehemu ambayo siyo Misikiti mitatu (Msikiti Mtukufu wa Makkah na Msikiti wa Mtume Madina na Masjidul Aqswaa)? .......................................................... 85
Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Hadithi hizi zifuatazo ni sahihi au ni za uongo anazuliwa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Mambo yatakapo kuwieni mazito basi ni juu yenu kuzuru makaburi) na (Mwenye kuhiji kisha asinizuru hakika amenihama (yuko mbali nami) na (Mwenye kunizuru na akamzuru Baba yangu Ibrahim ndani ya mwaka mmoja nimemdhaminia Pepo kwa Allah) na (Mwenye kunizuru baada ya kufa kwangu ni kama aliyenizuru katika uhai wangu) na (Mwenye kuitakidi katika jambo basi limemnufaisha) na (Fanyeni Tawassuli kwa

(utukufu) jaha yangu kwasababu jaha yangu mbele ya Allah ni kubwa) na (Mja wangu amenitii basi ninakufanya ni miongoni mwa wanaosema kukiambia kitu kuwa na kikawa) na (Hakika Mwenyezi Mungu ameumba viumbe kutokana na nuru ya Mtume wake Muhammad rehma na amani za Allah ziwe juu yake). ........................................................................ 86
Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Inajuzu kuzika maiti Misikitini na kujenga Misikiti kwenye makaburi?... 87
Swali/ Utakapo ulizwa: ni ipi Hukumu ya kuyajengea makaburi? ........................................................... 88
Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Mtume rehma na amani ziwe juu yake alizikwa Msikitini?............................ 89
Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake yupo hai kaburini mwake na kwamba hutoka kwa watu katika maulidi kwa kile kinacho semwa kuwa anahudhuria kama wanavyo itakidi baadhi yao?................................................... 91
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni nini Bidaa? Na ni zipi aina zake? Na ni ipi hukumu ya kila moja? Na je! Katika Uislamu kuna bidaa nzuri?....................................... 93
Swali/ Utakapo ulizwa: Inafahamikaje kauli ya Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake: (Mwenye kuweka Sunnah iliyokuwa nzuri anamalipo yake na malipo ya mwenye kuifanya Sunnah hiyo)?94
Swali/ Utakapo ulizwa: Inafahamikaje kauli ya Omar radhi za Allah ziwe juu yake: (Neema ya Bidaa) na kuzuka kwa Adhana ya pili siku ya Ijumaa wakati wa Othman radhi za Allah ziwe juu yake? .................... 95
Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume ni Sunnah au ni bidaa? ......................... 97
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi hukumu ya kujifunza uchawi, au kufanya kazi ya uchawi?........................ 99
Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Wanavyofanya watu wa mazingaombwe ya kujichoma (kwa visu) na kula vitu vigumu ni uchawi na mazingaombwe au ni makarama? ...................................................................... 100
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi hukumu ya kwenda kwa mchawi kwa ajili ya tiba?..................................... 102

Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi namna ya kujikinga kutokana na uchawi kabla haujakupata na ni ipi tiba yake ukikupata? .................................................... 102
Swali/ Utakapo ulizwa: Je! Inajuzu kwenda kwa kuhani na watu wa kutazamia nyota na wenye kusomea vikombe au kiganja na wenye kudai kwamba wana elimu ya mambo yajayo kwa unajimu (kutumia nyota) na kwamba wanajua mambo ya mawinguni? ......... 103
Swali/ Utakapo ulizwa: Unasema nini katika hadithi hii: (Jifunzeni uchawi wala msifanye uchawi)? ..... 105
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni watu gani ambao ni bishara bora baada ya Manabii? ......................................... 105
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni nini wajibu wetu kwa Maswahaba radhi za Allah ziwe juu yao na ni ipi hukumu ya kumtukana mmoja wao? ...................... 106
Swali/ Utakapo ulizwa: Ni ipi adhabu ya mwenye kumtukana mmoja kati ya Maswahaba wa Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake- au akamtukana mmoja kati ya wakeze Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake? ............................... 107
Swali/ Utakapo ulizwa: Je, inajuzu kusema kwamba watu wote ni dini moja? ........................................ 108
Swali/ Utakapo ulizwa: ni yapi matunda ya kumuamini Allah na kumpwekesha na kusimama (kuwa na msimamo) katika kufuata sunnah za Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake? ............................... 109
Hitimisho ............................................................... 112

# عقيدة الأئمة الأربعة رحمهم الله


# (أبو حنيفة ومالك والشافعي وابن حنبل)

(باللغة السواحيلية)

إعداد: نخبة من طلبة العلم

تقديم: صلاح بن محمد البدير

**ترجمة ومراجعة: مركز رواد الترجمة**




# Itikadi ya Maimamu wanne Mwenyezi Mungu awarehemu

ترجمة : رواد الترجمة